SportPesa
TZS. 576,086,780
BET LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mtanzania** anukia ukatibu wa Bunge la Afrika Mashariki

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Oktoba 16, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580735

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Zilivyokuwa saa 6 hukumu ya Sabaya

**AHUKUMIWA** kifungo miaka 30, mama mzazi atoka kabla ya hukumu, hakimu aondoa adhabu ya viboko... *Endelea uk. 2*



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (wa tatu kushoto) na wenzake, wakiteta jambo na Wakili wao, Mosses Mahuna, kabla ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha jana. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

## Samia asema mchakato wa Moshi kuwa Jiji bado kidogo

UKURASA 2



UKURASA 3

## Waziri Mkumbo asema saruji ipo ya kutosha

UKURASA WA 4

### RAIS MWINYI ASISITIZA KUDUMISHA MUUNGANO

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka Watanzania kuendelea kudumisha Muungano kwa kuhakikisha wananchi wanapata fursa...

UKURASA WA 4

### WHO YATOA RIPOTI YA UTAFITI CHANJO CORONA

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema nchi zilizofanya utafiti ambako chanjo ya Uviko-19 ipo juu, zimebaini asilimia zaidi ya 99.9 ya wagonjwa waliopata...

UKURASA WA 5

### MAJALIWA ATAKA RUBONDO ITANGAZWE

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ameliagiza Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ishirikiane na wadau wa masuala ya utalii ukiwemo uongozi wa kambi ya kupokea watalii...

**MICHEZO** **GOMES AFUNGUKA USHINDI NI LAZIMA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akiondoa kitambaa kuzindua rasmi barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 32.2, katika eneo la Sanya Juu, wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: IKULU**

# Zilivyokuwa saa sita hukumu ya Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imemtia hatiani na kumhukumu kifungo cha miaka 30 jela aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (34) na wenzake wawili.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine katika shauri hilo, ni Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura, waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Akisoma hukumu hiyo iliyochukua muda wa karibu saa sita jana, Hakimu wa Mahakama hiyo, Odira Amworo, alisema kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani, mahakama imewatia hatiani na kuwahukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kwa kutenda makosa hayo matatu.

Hakimu Amworo alisema kosa na kwanza na la pili ni la unyang'anyi wa makundi pasipo kutumia silaha, ambalo Sabaya na wenzake waliwatendea Numan Yasin na Ramadhani Rashi katika duka la Mohame Saad lililoko Mtaa wa Bondeni jijini Arusha.

Alisema kuwa kosa la tatu ni la unyang'anyi wa kutumia silaha ambalo washtakiwa hao walimtendea Bakari Msangi kwa kumpiga, kumfunga pingu, kumtishia kwa silaha na kumpora fedha Sh. 390,000.

Hakimu huyo, akisoma hukumu hiyo, alisema hakuna ubishi kwamba Sabaya akiwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mwenye mamlaka ya uteuzi, alitenda makosa hayo kinyume cha sheria.

Kadhalika, alisema kwa kuwa mikono yake imefungwa kutokana na sheria, hawezi kutoa adhabu za zaidi ya kifungo cha miaka 30 japokuwa wametiwa hatiani kwa makosa matatu na kila kosa ni miaka 30, hivyo watatumikia kwa pamoja.

Alisema kosa la kwanza, la pili na la tatu ni vifungo vya miaka 30 kwa kila kosa na wakati mwingine vifungo hivyo vinakwenda sambamba na adhabu ya viboko, lakini alikataa ombi la Wakili wa Jamhuri adhabu hiyo kutekelezwa sambamba na viboko.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, alidai kwamba washtakiwa hao hawakuwa na kumbukumbu wala rekodi ya kutenda makosa ya jinai ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Kwa kosa la kwanza na la tatu aliomba mahakama kutoa hukumu ya kuwafunga miaka 30 jela sambamba na kuchapwa viboko kama sheria inavyoelekeza.

Vilevile, kwa kosa la pili aliomba mahakama washtakiwa hao kuchwapwa vikoko kwa kuwa ni matakwa ya kisheria na hilo liko wazi.

"Tunaomba adhabu hii kali itendeke kwa kuwa Sabaya alikuwa mteule wa Rais na alifanya vitendo vya unyang'anyi wa kutumia silaha na kutumia makundi ni kinyume cha mamlaka iliyomteua ili iwe fundisho kwa wengine katika jamii hasa viongozi waliopewa dhamana na serikali na watu,"alidai Kwetukia.

Wakili huyo alidai kwamba utetezi wa umri kwa washtakiwa hao hauna mashiko katika kutaka kupunguziwa adhabu kwa kuwa walipaswa kufanya kazi ya kujipatia kipato halali pasipo kujiingiza katika vitendo vya uhalifu.

Baada ya maeleza hayo kutoka kwa Wakili wa Jamhuri, Wakili wa Mshtakiwa wa kwanza (Sabaya), Mosses Mahuna, alidai sheria imeeleza wazi ukitiwa hatiani kifungo ni cha miaka 30 na kinaweza kuambatana na viboko au vasiwapo.

"Tunaomba umwonee huruma mshatikiwa wa kwanza, hili ni kosa lake la kwanza na alikuwa mtumishi wa serikali na amelitumikia taifa hili, hivyo tunaomba mahakama kutoa adhabu ambayo imeangalia vizuri kwa kutambua huduma alizotoa katika jamii," alidai Mahuna.

Alidai kuwa mshtakiwa alitoa ushirikiano kwa vyombo vya dola wakati alipokamatwa na pia bado ni kijana mdogo na ni nguvu kazi ya taifa na endapo atafungwa kifungo cha miaka mingi, maisha yake yataishia gerezani, hivyo aliomba kupewa adhabu ya muda mfupi ili arejee uraiani kulitumia taifa.

"Familia, mke na watoto wanamtegemea, tunaomba adhabu iwe kwa pamoja kwa makosa yote, kwa kuwa adhabu ikiwa kwa kila kosa atafungwa miaka 90, tunaomba ikiwezekana iwe miaka 30 tu," alidai Mahuna.

Awali majira ya saa mbili asubuhi, wananchi walianza kufurika katika viwanja vya mahakama huku askari wakiwa wametapakaa kila kona ya viunga vya mahakama hiyo.

Hakimu aliingia katika viwanja vya mahakama majira ya saa 2:25 asubuhi kabla ya kuanza kutoa hukumu hiyo majira ya saa 5:57 asubuhi na kufikia tamati ya hukumu saa 11:47 jioni.

Baada ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Sabaya na wenzake walionekana kuwa na nyuso za huzuni na wenye hofu kubwa huku ndugu jamaa na marafiki wakionekana kusikitika.

Nipashe ilishuhudia mama mzazi wa Sabaya akitoka ndani ya chumba cha mahakama mapema kabla ya kusomwa kwa hukumu hiyo.

# Samia: Mchakato Moshi kuwa jiji bado kidogo

**Na Waandishi Wetu,** MOSHI

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewafungulia wakazi wa Mji wa Moshi kinachoendelea kuhusu Halmashauri ya Manispaa hiyo kupandishwa hadhi kuwa jiji, kwamba kuna mambo bado hayajakamilika.

Akizungumza jana na wakazi hao kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Rais Samia, alitolea ufafanuzi suala hilo kutokana na ombi la kuharakisha mchakato huo lililoibuliwa awali mkutanoni.

"Mji wa Moshi unadaiwa ili uwe Jiji, na Mji wa Vunjo nao wanataka kuwa Halmashauri, na kutoka Vunjo hadi Moshi ni takribani kilometa 20, Je, tuivunje Vunjo, iwe ndani ya litakalokuwa Jiji la Moshi?" Rais Samia alitamka katika ufafanuzi wake.

Aliahidi serikali kufanyia kazi suala hilo, katika hali inayoendana na ombi hilo lililoibuliwa mkutanoni na mmoja wa viongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Juzi, akiwa katika mkutano wa hadhara mjini Chato, Rais Samia alitoa ufafanuzi unaofanana na wa jana kuhusu mji huo wa Kanda ya Ziwa, katika mchakato wake wa kuwa mkoa.

Akiwa wilayani Siha jana, Rais Samia alizindua barabara ya Sanya Juu/Elerai iliyojengwa kwa kiwango cha lami na Kampuni ya Kimataifa ya Geo Engineering ya China (CGC), ikigharimu zaidi ya Sh. bilioni 62.7.

Kwenye taarifa ya utekelezaji ujenzi wa barabara hiyo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Rogatus Mativila, alisema ujenzi wa barabara hiyo ulikamilika mwaka 2019 na inatarajiwa kudumu kwa wastani wa miaka 20.

Rais Samia Suluhu Hassan alisema tatizo kubwa lililoko Mkoa wa Kilimanjaro ni migogoro ya ardhi, huku akiahidi kuitatua haraka.

Alisema matatizo yote ambayo ameyaona kwenye mabango yenye jumbe mbalimbali ikiwamo migogoro ya ardhi, maji na maslahi ya wafanyakazi, ameyachukua na anakwenda kuyachambua na kuyafanyia kazi.

"Tunapita kuangalia yaliyotendeka na kuona matatizo yaliyopo na hapa ninaona mabango mengi. Kuna migogoro ya ardhi na maslahi ya wafanyakazi, ninaomba tuyakusanye yote halafu tutaenda kuyafanyia kazi.

"Changamoto hizi tutaenda kuzifanyia kazi na ahadi yetu Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni kuangalia kero za wananchi na kuzifanyia kazi.

"Ninajua hapa Kilimanjaro kuna changamoto ya maji na migogoro ya ardhi ambayo ndio changamoto kubwa. Changamoto zote ambazo nimeziona kwenye mabango nitazichukua na kwenda kuzichambua na kuzifanyia kazi," alisema.

Vilevile, Rais Samia alisema baadhi ya wananchi wapo kwenye maeneo ya serikali na wanatakiwa kuondoka, akiahidi kuangalia namna bora ya kushughulikia dosari hiyo.

Rai yake kwa wakazi wa Kilimanjaro, waendelee kudumisha amani na utulivu ili serikali ipate wasaa wa kuangalia namna nzuri ya kushugulikia vikwazo vilivyopo.

**■Imeandikwa na Godfrey Mushi na Anjela Mhando***



Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo (wa pili kushoto), akikagua na kupokea maelezo ya uzalishaji ya kiwanda cha saruji cha Twiga, alipotembelea kiwandani hapo, eneo la Wazo, mkoani Dar es Salaam jana, ili kujua hali ya upatikanaji na uzalishaji wa bidhaa hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Mkumbo asema hakuna upungufu wa saruji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amewatoa hofu wananchi kwamba hali ya upatikanaji wa saruji nchini ni ya kuridhisha na viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo kwa sasa vinatosheleza uhitaji wa nchi.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo jana alipotembelea Kiwanda cha Saruji cha Twiga, Dar es Salaam ili kujiridhisha na uzalishajii na upatikanaji wa saruji.

Ziara hiyo inatokana na Tanzania kunufaika mkopo wa Sh. trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) ambazo zitatumika katika kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo kuboresha huduma za jamii katika sekta za afya, elimu, utalii na maji.

"Niwahakikishie Watanzania hali ya upatikanaji wa saruji nchini ni mzuri kulingana na uhitaji wa saruji na viwanda tulivyonavyo hakuna changamoto" alisema Prof. Mkumbo

Prof. Mkumbo alisema kuwa hali ya umeme katika viwanda inaendelea kuboreka lakini bado kuna changamoto kidogo.

Kutokana na hali hiyo, alisema atakutana wa Waziri wa Nishati, January Makamba ili kuhakikisha tatizo la umeme katika kiwanda cha Twiga na viwanda vingine nchini linakwisha kabisa.

Prof. Mkumbo pia alikutana na kufanya mazungumzo na mjumbe wa kampuni iliyowekeza katika kiwanda hicho kutoka Ujerumani ili kujadili maendeleo ya kiwanda na kumpa uhakika kuwa serikali ya Tanzania inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji wao ambao wamefanya na wanaendelea kupanua.

# Mtanzania anukia ukatibu Bunge la Afrika Mashariki

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WABUNGE wa Uganda wanataka utaratibu wa kuajiri watumishi wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) usitishwe baada ya mgombea wao katika nafasi ya Katibu wa Bunge hilo kudaiwa kuzidiwa katika usaili na Mtanzania.

Katika hali isiyo ya kawaida, wabunge wa Uganda juzi waligoma kuingia kwenye Ukumbi wa EALA jijini Arusha wakidai kutoridhishwa na utaratibu mzima wa kumpata Katibu wa EALA - nafasi ya juu kabisa kwa waajiriwa katika chombo hicho cha kutunga sheria katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Hata hivyo, taarifa kutoka ndani ya Bunge hilo zinadai kuwa uamuzi wa wabunge hao kutoka Uganda umetokana na kuvuja kwa taarifa kuwa mgombea kutoka Tanzania, Saidi Othman Yakubu, ndiye aliyeongoza kwa kufanya vizuri katika usaili kumzidi Alex Lumumba Obatre kutoka Uganda.

Maana ya matokeo hayo ni kwamba Mtanzania huyo anapewa nafasi kubwa ya kuwa Katibu wa EALA ikiwa ni mara ya kwanza kwa raia wa Tanzania kushika wadhifa huo tangu kufufuliwa kwa EAC mwaka 1997.

Katibu mpya wa Bunge hilo anakwenda kuchukua nafasi ya Kenneth Madete kutoka Uganda, aliyeshika wadhifa huo kuanzia mwaka 2009 hadi mwaka 2019. Kabla ya kuwa Katibu, Madete alikuwa Naibu Katibu kuanzia mwaka 2001 hadi mwaka 2009.

Obatre ambaye anadaiwa kushindwa na Yakubu katika usaili huo, alikuwa Naibu Katibu wa EALA kuanzia mwaka 2009 hadi mwaka 2019. Kwa maana hiyo, kati ya mwaka 2009 hadi mwaka 2019, Uganda ilikuwa na Katibu na Naibu wake katika nafasi hiyo nyeti kwenye chombo hicho.

"Ninafikiri kinachotusumbua ni ubinafsi tu katika hili. Wamekuwa katika nafasi hizi kwa takribani miaka 20 na katika miaka 10 iliyopita wao ndiyo walikuwa na nafasi zote. Leo kashinda Mtanzania wanataka jambo hili libadilishwe ili apewe wao. Kwani cheo hicho kipo kwa ajili ya Waganda peke yao?" alihoji mmoja wa wabunge wa EALA katika mazungumzo na Nipashe jana jijini Arusha.

Yakubu, mwanasheria aliyepata mafunzo yake Uingereza, ana uzoefu wa kibunge wa zaidi ya miaka 15; akiwa amehudumia katika nafasi tofauti katika Bunge la Tanzania pamoja na nyadhifa nyingine katika jamii ya kimataifa. Baada ya wabunge wa Uganda kugomea kikao cha juzi, ilibidi Spika wa Bunge la EALA, Martin Ngoga, aahirishe kwa sababu akidi ya kufikia uamuzi wa vikao haikuwa imefikiwa kutokana na taratibu za Bunge hilo.

Kikao kingine cha EALA kimepangwa kufanyika Jumanne ijayo. Hivi karibuni, EALA ilitangaza nafasi za kazi 46 katika idara mbalimbali zilizo chini yake na kwa mujibu wa taarifa iliyowekwa hadharani na taasisi hiyo, jumla ya waombaji 311 kutoka nchi wanachama walijitokeza kuwania nafasi hizo, wakiwamo Watanzania 84.

Hatua hiyo ya wabunge wa Uganda tayari imeanza kuzua mijadala katika mitandao ya kijamii na watu mashuhuri, wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa, wameanza kutoa maoni yao kuhusu namna ya kutatua sintofahamu iliyopo.

Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alitumia ukurasa wake rasmi wa mtandao wa kijamii wa Twitter kumwomba Rais Yoweri Museveni wa Uganda, kuingilia kati jambo hilo na kuwataka wabunge kutoka taifa lake wawe wazalendo na kuruhusu watu wa nchi zingine wapate fursa ya kuhudumia Bunge hilo. "Jambo hili halina sababu ya kuzusha mgogoro. Ninamwomba Rais Museveni wa Uganda awaambie wabunge wake waachane na mambo ya mgomo na wawape nafasi wana Afrika Mashariki wengine nao wahudumie chombo hicho," alisema.


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

**TANGAZO LA KUAHIRISHA MNADA WA HADHARA WA MAGARI**

Wananchi wote wanatangaziwa kwamba Mnada uliokuwa umepangwa kufanyika Jumamosi tarehe 16/10/2021 umeahirishwa hadi mtakapo tangaziwa tarehe nyingine ya Mnada. Tunaomba radhi kwa usufumbufu utakaojitokeza.

**MKURUGENZI MKUU**
**KAMPUNI YA NDEGE TANZANIA (ATCL)**

216516902

# WHO yatoa ripoti ya utafiti chanjo corona

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema nchi zilizofanya utafiti ambako chanjo ya Uviko-19 ipo juu, zimebaini asilimia zaidi ya 99.9 ya wagonjwa waliopata ugonjwa mkali ni wale ambao hawachanja na kuwataka wananchi waendelee kuchanja.

Mtaalamu anayeshughulikia matatizo ya corona na kujikinga dhidi ya janga hilo, Dk. Nemes Iriya, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano na waandishi wa habari kuhusu hali ya mwelekeo wa ugonjwa huo na uchanjaji nchini.

Dk. Iriya alisema utafiti huo umeonyesha ni mtu mmoja katikati kila kundi la watu milioni moja anayepata ugonjwa wa Uviko-19 wakati akiwa ameshachanja.

"Hakuna dawa tunayosema hii inatibu Uviko-19, zilizopo zinapunguza makali ya ugonjwa huu na kuzuia kupunguza vifo kwa kiasi kikubwa, ili tusipate watu wengi kuingia kwenye ugonjwa mkali na vifo ndio maana chanjo imeletwa.

"Chanjo inapunguza kwa kiasi kikubwa watu wanaopata ugonjwa huu kuwapekea kupata ugonjwa mkali na kusababisha vifo," alisema.

Dk. Iriya alisema chanjo inapunguza wingi wa wadudu katika njia ya hewa na kuambukiza mtu kwenda kwa mtu.

Alisema gharama za matibabu ya ugonjwa huo ni kubwa, hivyo Watanzania wanatakiwa kujikinga ipasavyo kwa kupata chanjo.

Mwakilishi Mkazi wa WHO Tanzania, Dk. Tigest Mengestu, alisema kupungua kwa maambukizi ya Uviko-19 kunatoa nafasi kwa watu ambao hawajachanja kufanya hivyo ili kuongeza kinga miongoni mwa jamii.

Alisema lengo ni kufikia asilimia 60 ya waliochanja Tanzania ili kutengeneza kinga kamili kwa jamii.

Dk. Mengestu aliipongeza serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha kampeni ya chanjo ambayo wanaona imezaa matunda na hali ya uchanjaji inaimarika.

"WHO na wadau wengine wa afya Tanzania tunaunga mkono serikali katika ngazi ya mkoa na wilaya na katika vituo vya afya ili kuboresha ubora wa huduma ya chanjo ya Uviko-19," alisema.

Mtaalamu wa chanjo WHO, Dk. William Mwengee, alisema kulingana na takwimu ambazo wamekuwa wakizipokea kutoka serikalini, wanaona zinatoa matumaini kwa sababu zinaonyesha kwa sasa hali ni shwari.

Alisema ni wakati sahihi kwa ambao bado hawajachanja, wachanje kabla ya wimbi lingine halijaibuka.

# Mwinyi asisitiza kudumisha Muungano

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka Watanzania kuendelea kudumisha Muungano kwa kuhakikisha wananchi wanapata fursa ya kufanya biashara bila bughudha yoyote.

Dk. Mwinyi alisema hayo wakati akizindua miradi minne ya Jeshi la Magereza iliyoko mkoani hapa.

Akizindua miradi hiyo, Dk. Mwinyi alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumpa nafasi ya kufanya kazi hiyo ambayo ni kwa miradi ya Ngome ya Gereza la Mkono wa Mara, jengo la huduma ya afya ya mama na mtoto, nyumba za makazi ya maofisa na askari pamoja na kiwanda cha maziwa cha Kingolwira kwa niaba yake.

Pia alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais Samia kwa jitihada zake za kuwaletea maendeleo wananchi. Rais Mwinyi alisema mongoni mwa faida ya Muungano ni wananchi wa pande zote mbili wamekuwa wakifanya biashara ikiwamo ya mchele.

"Walaji wakubwa wa mchele ambao mwingi unatoka Tanzania Bara ikiwamo Morogoro wako Zanzibar, hivyo tuendelee kudumisha Muungano wetu kuhakikisha wananchi wetu wanapata fursa ya kuendelea kufanya biashara bila bughudha yoyote," alisema.

Kuhusu miradi ya Jeshi Magereza, Dk Mwinyi alisema kwa mujibu wa Kamishna Jenerali wa Jeshi hilo, ni sehemu ya miradi mingi inayoendelea kutekelezwa na chombo hicho ndani ya mkoa huo na maeneo mbalimbali nchini.

Alisema hatua ya Jeshi la Magereza kuwa na ubunifu wa miradi mbalimbali ya maendeleo inafaa kuigwa kwa kuwa ni kielelezo kizuri kwa taasisi zingine kujiongeza na kujipatia kipato kutoka kwenye miradi yao pamoja na kuimarisha ustawi wa maisha ya wananchi ya kuwapatia huduma mbalimbali.

Nampongeza Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuiwezesha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia Jeshi la Magereza " alisema.

"Nawapongezeni viongozi wa Jeshi la Magereza kwa usimamizi mzuri wa fedha za miradi hii kama tulivyosikia hivi punde karibu asilimia 75 ya fedha zinatoka serikali kuu kuiwezesha Magereza lakini asilimia 25 ni fedha za ndani ya jeshi jambo ambalo ni la kuigwa na taasisi zingine " aliongeza.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alisema jeshi hilo limepewa jukumu la kujenga uwezo wa kujitengemea kwa chakula.

Simbachawene alisema Jeshi hilo kwa sasa lina uwezo wa kulisha wafungwa na mahabusi kwa asilimia 100 kwa kipindi cha mwaka mmoja na miezi sita na limeokoa takribani Sh. bilioni moja kwa mwezi ambapo kwa mwaka ni zaidi ya Sh. bilioni 12 zilizokuwa zinatolewa na serikali.

Pia alisema Jeshi hilo katika mikakati ya maboresho limejenga nyumba mpya za makazi ya askari na maofisa zipatazo 400 na nyingine bado zinaendelea kujengwa nchi mzima.



Ofisa Mtendaji wa Kata ya Tandika, Manispaa ya Temeke, Hijja Kipeleka (aliyeshika kitabu), akitoa maelekezo kwa wafanyabiashara wa Soko la Tandika kwa Mpochea, mkoani Dar es Salaam jana, wakati wa ugawaji wa vizimba kwa ajili ya wafanyabiashara maeneo ya barabara "Machinga". **PICHA: DEVOTA MWACHANG'A**

# Wanachama wa Ushirika wapewa angalizo SACCOS

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), amewataka wanachama wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kusimamia, kufuatilia mali na uendeshaji wa shughuli za vyama vyao ili kuongeza tija na ukuaji wake nchini.

Prof. Alfred Sife aliyasema hayo juzi kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Prof. Aldolf Mkenda, kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Duniani (ICUD) yaliyofanyika wilayani hapa.

Aliwataka wanachama kutimiza wajibu wao kwa kushiriki kupata viongozi bora wa vyama, kutoa huduma zenye ubunifu na uadilifu katika utendaji.

Kiongozi huyo aliwataka wanaushirika kuwa makini katika uwekezaji bora wa rasilimali za vyama vyao vya ushirika.

"Serikali kwa kutambua umuhimu wa Sekta ya Ushirika hasa ushirika wa kifedha imekuwa ikichangia maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Niwahakikishie kuwa tutasimamia ushirika kwa kuzingatia sheria na kuhakikisha kuwa hautetekeleki," alisema Prof. Sife.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, aliwataka wanachama wa vyama hivyo kufuatilia utendaji wa vyama vyao ili kuhakikisha usimamizi unaimarika katika vyama na hati safi za ukaguzi zinaongezeka.

"Mtu wa kwanza wa kuhakikisha chama kinapata hati safi ni mwanachama wa chama cha ushirika kwa kufika kwenye mikutano inapoitishwa, kushiriki kwenye uamuzi wenye maslahi kwa chama, ni lazima tubadilike na kusimamia mali zetu nguvu ya ushirika lazima ianzie kwa wanachama wenyewe," alisema Mrajis.

Aidha, Mrajis alisema ni wakati sahihi sasa kwa vyama vya ushirika wa mazao kuwa na vyama vya akiba na mikopo ili kuongeza mzunguko wa fedha kwa wakulima hasa kuwawezesha kumudu gharama mbalimbali za kilimo wakati wa misimu ya mazao.

Dk. Ndiege alitoa rai kwa vyama ambavyo bado havijaomba leseni za uendeshaji wa SACCOS kwa mujibu wa Sheria Na. 10 ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018, kufanya hivyo ili kuendana na matakwa ya sheria, kanuni na taratibu zinazolenga kuongeza ufanisi wa vyama.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SCCULT), Dk. Gervas Machimu, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuwaenzi na kukumbuka mchango wa waasisi wa vyama hivyo, wanaushirika kukaa pamoja kubadilisha uzoefu na kutathmini mchango wa SACCOS katika maendeleo ya nchi.

Mwenyekiti huyo alishauri SACCOS kuendelea kushiriki katika michakato ya mabadiliko ya sheria pamoja na mapitio mengine ya maboresho na mabadiliko ya mifumo ya ushirika nchini.

## HABARI KITAIFA




Mkurugenzi wa Biashara ya Mafuta na Gesi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC), Dk. Hudson Willington (katikati), akizungumza katika Mkutano Mkuu wa TPDC SACCOS Ltd, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mwenyekiti wa TPDC Saccos, Renatus Kachira na Ofisa Ushirika wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Donald Kibhuti. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Majaliwa ataka Rubondo itangazwe

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ameliagiza Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ishirikiane na wadau wa masuala ya utalii ukiwemo uongozi wa kambi ya kupokea watalii ya Asilia kuitangaza hifadhi ya kisiwa cha Rubondo.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akizungumza na baadhi ya watumishi wa TANAPA na wa kambi ya Asilia Rubondo akiwa katika ziara fupi ya kuhamasisha utalii katika hifadhi ya Kisiwa Rubondo, mkoani Geita.

Alisema ili sekta hiyo ipate tija, uongozi wa TANAPA unapaswa kuwa karibu na wadau wa masuala ya utalii.

"Endeleeni kuwasikiliza na kushirikiana nao katika kutatua changamoto zinazowakabili ili kuongeza idadi ya watalii," alisema.

Majaliwa pia aliupongweza uongozi wa kampuni ya Asilia kwa uwekezaji wake katika sekta ya utalii nchini na ameusisitiza uendelee kupanua wigo ili kukuza sekta hiyo na kuongeza tija.

Naibu Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA Kanda ya Magharibi, Martine Loibooki, alimshukuru Waziri Mkuu kwa hatua yake ya kuhamasisha utalii katika hifadhi ya Rubondo na kwamba watayafanyia kazi maelekezo yote aliyoyatoa.

Hifadhi ya Kisiwa cha Rubondo ina ukubwa wa kilometa za mraba 457, iko kaskazini magharibi mwa Tanzania ndani ya Ziwa Victoria, ziwa ambalo ni la pili kwa ukubwa duniani. Hifadhi hiyo inaundwa na visiwa vidogo 11 kikiwamo na kisiwa cha Ndege.

Kisiwa cha Rubondo ndilo eneo pekee katika Ziwa Victoria lenye mazalia ya samaki yaliyohifadhiwa kisheria. Samaki wanaopatikana katika kisiwa hicho ni pamoja na sato na sangara ambao wanaweza kukua hadi kufikia uzito wa kilo 100.

Fukwe za kisiwa hicho ni miongoni mwa makazi ya pongo na nzohe. Pia hifadhi hiyo ni maskani makuu ya mamba, ndege na samaki kama zumbuli, chechele na taisamaki. Mbali na ndege hao kisiwa hicho ni makazi ya aina nyingi za ndege wa majini na mimea kadhaa ambayo hutoa harufu nzuri ya kuvutia.

Wanyama wakazi wa hifadhi ya Rubondo ni pamoja na viboko, pongo, nzohe, fisi maji, mamba na pimbi wanashirikiana makazi na wanyama waliohamishiwa katika hifadhi hiyo kama sokwe, tembo, mbega weusi na weupe na twiga.

Pia, aina nyingine ya utalii inayofanyika katika hifadhi hiyo ni pamoja na uvuvi wa samaki wa kitalii (sport fishing).

# Makandarasi waonywa kulipua kazi

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MBUNGE wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, amewaonya makandarasi ambao wanatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo mjini humo, kuwa atakayevuruga hatapata kazi tena.

Katambi ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, na Ajira, alibainisha hayo jana wakati akikagua ujenzi wa madaraja matatu mjini hapa.

Alisema, serikali inatumia fedha nyingi kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi, hivyo hatarajii kuona miradi hiyo inajengwa chini ya kiwango na kubainisha kuwa mkandarasi atakaevuruga kazi zake hatapewa tena kazi.

"Nimekagua ujenzi wa madaraja matatu la Uzogole ambalo limegharimu Sh. milioni 190, Iwelyangula Sh. milioni 428 na daraja wa watembea kwa miguu la Upongoji Sh. milioni 100. Fedha hizi ni nyingi na sitarajii yawe chini ya kiwango," alisema Katambi.

"Natoa ujumbe kwa makandarasi ambao wanatekeleza ujenzi wa madaraja haya matatu na miradi mingine. Watakaotekeleza chini ya kiwango hawatapata kazi tena, labda nikose ubunge. Nataka miradi hii ihudumie wananchi kwa muda mrefu," aliongeza.

Katika hatua nyingine, Katambi alisema wataendelea kukarabati marabara za Manispaa ya Shinyanga kwa kiwango cha changarawe pamoja na ujenzi wa vituo vya afya na vyumba vya madarasa.

Baadhi ya wanafunzi ambao wanasoma katika Shule ya Sekondari Chamaguha, walishukuru ujenzi wa daraja hilo jipya la Iwelyangula ambapo daraja la awali lilisombwa na maji, hivyo mvua ikinyesha kushindwa kwenda shuleni.

Naye Kaimu Meneja Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Manispaa ya Shinyanga, Yohana Marwa, alisema ujenzi wa madaraja hayo matatu unaendelea vizuri na mengine yameshakamilika kwa asil-


# NOTISI/ TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, ,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| AGGREY | HAWA LEONARD MLUNYA | GARI TOYOTA IST T579 DED | MGENYI BADRU MAHMOOD | TABATA CHAMA | 30/10/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | STAFORD CHRISTOPHER SENYE /JUNIOUR & ANDREW BUSINESS | NYUMBA | STAFORD CHRISTOPHER SENYE | MKURANGA | 05/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | NEEMA CLEMENCE NKYA | NYUMBA | JULIANA INVOCAVITY MUSHI | KIMARA-KIBO | 30/10/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | NATHAN MASUMBUKO NDANGA | KIWANJA | NATHAN MASUMBUKO NDANGA | MKURANGA | 05/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ESTHER BENAD KULWIJIRA | NYUMBA | PAUL JULIUS MUHIRI | KIPUNGUNI | 09/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ASNATI ATHUMANI RAJABU | NYUMBA | ASNATI ATHUMANI RAJABU | SARANGA | 12/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | LEONARD BAKUZA KABILO | NYUMBA | LEONARD BAKUZA KABILO | VIWEGE MAJOHE | 15/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ONESMO PETER MASIMA | NYUMBA | ONESMO PETER MASIMA | UKONGA MAZIZINI | 10/11/2021 SAA TANO ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | SALUM OMARY MTENGWA | NYUMBA | RAMADHANI NASSOR BOMBWE | BUGURUNI | 17/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MASUDI JUMANNE RAMADHANI | NYUMBA | BEATRICE STEPHANO KISHERU | SARANGA | 18/11/2021 SAA TANO ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | SHARIFA SAIDI HAMISI | NYUMBA | SHARIFA SAIDI HAMISI | PUGU BOMBANI | 24/11/2021 SAA TANO ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | JULIUS RYOBA DANIEL | NYUMBA | JULIUS RYOBA DANIEL | KITUNDA MZINGA | 10/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | VAILETH ERASTO TWEVE | NYUMBA | JOSEPH BENEDICT/VAILETH ERASTO | KITUNDA KATI | 10/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | NEEMA ARON URIO | NYUMBA | OMARY ATHUMAN MKINDI | KISIWANI-KIGAMBON | 12/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA MBILI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | FOREST MBEYA NA TUNDUMA | 05/11/2021 SAA TANO ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | OMARY SAIDI OMARY | NYUMBA | MIZE MASOUD HASSANI | MIKWAMBE | 04/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | JULIUS FRANSIS MARWA | NYUMBA | MONICA LAURENT KASIGWA | KINONDONI- | 16/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA |
| UBUNGO | MKONDA HOUSE OF FOOD | NYUMBA | PAMELA MACHIRA NYITAMBE | TABATA KIMANGA | 23/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | MATHIAS EUSEBIO MBONDE | NYUMBA | MATHIAS EUSEBIO MBONDE | KIMARA STOP OVER | 11/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | JOYCE MARIJANI MSOFE | NYUMBA | JOYCE MARIJANI MSOFE | KIMARA | 09/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | GOODLUCK JEROME TARIMO | NYUMBA | JOSEPH REUBEN MATARI | BOKO MAGENGENI | 13/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | ATHUMAN HASSAN HEMEDI | NYUMBA | ATHUMAN HASSAN HEMEDI | ULONGONI 'B' | 17/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MWANAHAMISI KONDO MATAMBO | NYUMBA | MWANAHAMISI KONDO MATAMBO | RUVU DARAJANI | 19/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | MALIKI MOHAMED MADIGADI | NYUMBA | MALIKI MOHAMED MADIGADI | VIKINDU | 09/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | HOPE ARTHUR MASAKA | KIWANJA | VENANCE RWEGOSHORA MUTAYOBA | KIBADA | 10/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | ELINEMA EMMANUEL KALALU | NYUMBA | ELINEMA EMMANUEL KALALU | MBAGALA | 17/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | JULIUS SIMBO LEMA | NYUMBA | HUSSEIN MTOBA FUNGALINDO | KINYAMWEZI DAMPO | 11/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | KHADIJA HUSSEIN JAFARAH | NYUMBA | JOACHIM MKWAVI | MBEZI MTONI | 23/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | JONATHAN AMAN ZAKAYO | NYUMBA | AMAN BRIAN ZAKAYO | MBEZI LUGURUNI | 16/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | HASSANI SADICK HILALI | NYUMBA | HASSANI SADICK HILALI | TUANGOMA - TEMEKE | 04/10/2021 SAA 04:00 ASUBUHI |
| BUGURUNI | SEIF HAMAD NASSORO | NYUMBA | SEIF HAMAD NASSORO | KILUNGULE | 04/10/2021 SAA 04:00 ASUBUHI |
| MAIN | AISHA HAMADI KIVINA | NYUMBA | AISHA HAMADI KIVINA | KIVULE MAJOHE | 04/10/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0765999000 /0715363537/ 0754497396/ 0784252048 /0714939933/ 0768672367
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

21657101

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri Simba, Azam, Biashara michuano ya CAF

**MECHI** za mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), zinatarajiwa kuendelea wikiendi hii.

Tanzania imebakiwa na timu tatu ambazo ni Simba ya jijini Dar es Salaam inayoshiriki Ligi ya Mabingwa wakati Azam FC ya jijini na Biashara United yenye makazi yake Musoma mkoani Mara zenyewe zinapeperusha bendera ya nchi katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Timu hizo zinacheza raundi ya kwanza, na Simba yenye mechi mbili tu mkononi baada ya hapo kama itapata matokeo mazuri itatinga hatua ya makundi kesho Jumapili itakuwa ugenini kuwavaa Jwaneng Galaxy ya Botswana wakati Azam leo inawakaribisha Pyramids kutoka Misri.

Biashara United inayonolewa na Mkenya yenyewe ilishuka dimbani jana kupambana na Al Ahly Tripoli na watarudiana ifikapo Oktoba 24, mwaka huu huko nchini Libya.

Tanzania ilipata nafasi nyingine ya kuwakilishwa na timu nne katika michuano hiyo ya CAF baada ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba kufika hatua ya robo fainali kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita.

Mbali na Yanga iliyoondolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Rivers United ya Nigeria, mabingwa wa Zanzibar, KMKM na Mafunzo nazo zilitolewa mapema kwenye michuano hiyo ya CAF kwa kufungwa mechi za nyumbani na ugenini.

Ili kuendelea kuzipata nafasi hizo, ni wazi wawakilishi hao watatu waliobakia wakapambana kusaka matokeo chanya na kusonga mbele.

Endapo timu hizo tatu zilizobakia, zitafuata nyao za Yanga iliyotolewa mapema, basi ni wazi msimu ujao wa 2022/23 nchi itarudi kule kule kwenye tiketi mbili, bingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwenda kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na mshindi wa Kombe la FA kupata nafasi ya kushiriki Kombe la Shirikisho Afrika.

Tunaamini wawakilishi hao watatu waliobakia watacheza mechi zao kwa utulivu na umakini na hatimaye kuendelea kuipa nchi pointi kwenye msimamo unaoandaliwa na CAF.

Macho yote ya mashabiki wa soka na michezo yako kwa Simba, Azam FC na Biashara United, kwa kuziombea dua njema ili wapate matokeo chanya na hatimaye kusonga mbele.

Nipashe inaamini wachezaji, viongozi na makocha wa timu hizo wanafahamu umuhimu wa kupata matokeo chanya kwenye michuano hiyo, ambapo mbali na kulitangaza vyema taifa, lakini binafsi watajiweka kwenye soko na vile vile watanufaika kiuchumi kutokana na mgawo wa fedha watakaopokea.

Kwa upande wa wachezaji, hii ni nafasi nyingine muhimu ya kutangaza vipaji vyao kwa sababu mechi za mashindano hayo ya kimataifa hufuatiliwa na mawakala na makocha kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Ni eneo muhimu la kujiweka sokoni na hatimaye kutimiza ndoto za kusajiliwa na klabu za nje, kama ilivyokuwa kwa Mbwana Samatta na msimu sasa Clatous Chama na Luis Miquissone wakisajiliwa baada ya kufanya vyema kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa walipokuwa na Simba.

Pia huu ni wakati mwingine wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kukaa karibu na klabu hizi na kuwasaidia kutatua changamoto walizonazo (kama zipo) na hatimaye kuona wachezaji wao wanaingia uwanjani kwa kazi moja ya kusaka ushindi.

Tunawakumbusha dunia ya sasa timu inaweza kupata ushindi ikiwa nyumbani au ugenini, lakini tunawaombea dua njema zaidi wawakilishi wetu wafanye vyema kwenye michezo yao ya kwanza na watakaporudiana iwe kazi rahisi au wakamilishe pale walipoishia.

**Mungu Ibariki Simba SC, Azam FC na Biashara United.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Uchongwao huchongewa paa...

Na Barnabas Maro

**"UCHONGWAO"** huchongewa paa ulimwengu ukamsawaa." Maana yake mti uliochongwa kwa nia ya kutumiwa katika paa huweza ukaishia kumchoma au kumfuma binadamu.

Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu aliyeufanya ubaya fulani akiudhamiria mtu mwingine halafu ukamrudia yeye mwenyewe. Tunasihiwa kutowatendea wenzetu mabaya.

Kadhalika husemwa: "Ufalme ni kama mvua hupiga na kupita." Methali hii hutumika kwa mtu anayejitapa kutokana na hali yake ya uchumi; anapaswa kujua kuwa hali hiyo haitadumu milele.

Timu za kandanda zina watu wenye nia tofauti. Wapo wanachama yaani watu wenye mapenzi ya dhati yaliyowafanya wanunue kadi za uanachama ambao hushiriki mikutano ya vilabu kwa mujibu wa katiba ya vilabu vyao.

**Timu za kandanda zina watu wenye nia tofauti. Wapo wanachama yaani watu wenye mapenzi ya dhati yaliyowafanya wanunue kadi za uanachama ambao hushiriki mikutano ya vilabu kwa mujibu wa katiba ya vilabu vyao.**

Wanachama ni watu walioijiunga na kikundi fulani cha watu wenye lengo maalum; waliojiunga na jumuiya au chama fulani. Hapa ndipo tunapopata majina tofauti za timu za kandanda, kama Azam, Biashara United, Dodoma Jiji, Geita Gold, Simba, Yanga na kadhalika.

Itokeapo vilabu kuwa na shida fulani inayohusu fedha ili kupambana na shida hiyo, wanachama huitwa kwenye mkutano maalum kujadili suala hilo. Matokeo yake ni wanachama kuchangishana fedha ili kukabiliana na hali hiyo.

Kadhalika kuna wasiokuwa wanachama ambao huitwa mashabiki. Hawa ni watu wenye mapenzi na hamasa kubwa kuhusu jambo au kitu fulani. Katika mashabiki 10 haishangazi kuwa katika hao ni wawili tu wanaoipenda timu kwa dhati yaani umakini wa moyo, nafsi ya kitu, jambo au mtu; mtu anayependa sana kitu. Kwa hiyo mashabiki ni wapita njia tu, leo wanapita njia hii na kesho njia tofauti kabisa.

Nafasi ya tatu ni wale wanaoitwa "wapita njia" yaani wanaofuata timu zinazoshinda tu. Zinaposhindwa, husambaratika, yaani vurugika. Kwa ufupi ni kitendo cha kutawanyika na kuvunjika mshikamano wa watu, vitu au mambo.

Hapa tunapata methali isemayo: "Bora kupigwa dhoruba ya dhahiri kuliko ya siri." Maana yake ni afadhali kufanyiwa ubaya wa wazi kuliko wa siri. Ukiwa wazi mtu huweza kupata usaidizi kutoka kwa watu wengine.

"Nasihi" ni kitendo cha kumshauri mtu na kumwelekeza afanye mambo mema (sihi). 2, kitendo cha kumsemesha mtu kwa upole na kwa maneno mazuri ili aridhie jambo analoambiwa.

Natoa nasaha kwa wanaopenda mpira wa miguu humu nchini kuwa: "Cha kichwa kitamu cha mkia kitamu." Maana yake kitu ambacho ni kizuri huwa kizuri chote kama ilivyo kitu kibaya hakiwi kibaya nusu na kizuri nusu.

Methali hii yatufunza tusiwe na tabia ya kigeugeu, ni vizuri kuwa na msimamo. Watu wa aina hii wanapaswa kutambua kuwa "Hakuna mume wa waume." Kwamba hakuna mtu mmoja anayeweza kuwashinda wanaume wenzake wote.

Methali hii huweza kutumiliwa mtu anayejitia ubabe au anayejidai kuwa na nguvu kama njia ya kumnyamazisha.

Kumbe ndio maana wahenga walisema: "Penye wengi pana mengi." Maana yake mahali ambapo pana watu wengi aghalabu huwa pana mambo mbalimbali.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

## HABARI KITAIFA

# CHAVITA yataka wataalamu wa lugha ya alama

**Na Christina Haule,** MOROGORO

CHAMA cha viziwi Tanzania (CHAVITA) Mkoa wa Morogoro, kimeishauri serikali kuona umuhimu wa kuweka wataalamu wa lugha ya alama kwenye matukio na maeneo mbalimbali muhimu kama vile hospitali ili wapate huduma stahiki.

Katibu wa CHAVITA Mkoa wa Morogoro, Salum Ally, alisema jana kuwa wamekuwa wakikabiliwa na ukosefu wa huduma muhimu hasa kusikilizwa wanapotaka kupata matibabu pindi wanapougua.

Alisema hali hiyo husababisha kutoa siri zao kwa watu wengine ili kuwafikishia kwa madaktari au wauguzi ndipo wapate huduma.

"Utakuta kiziwi anaumwa anaenda hospitalini daktari hawezi kumwelewa na anampa dawa wakati mwingine si za ugonjwa wake. Tumewaelekeza kurudi ofisi za chama kama wana wasiwasi au matatizo na akirudi tutalazimika kumtafuta mtu ili amweleze na warudi nae kwa daktari amwelezee na atapewa dawa sahihi," alisema.

Ally aliitaja changamoto nyingine kuwa ni mawasiliano hasa pale wanapokuwa viongozi wakubwa kwenye mikutano na kutoa maagizo ambayo hawasikii hali. Alisema husababisha wakati mwingine kukamatwa kwa kutenda kosa ambalo lilizuiwa bila wao kujua.

"Mfano anapokuja waziri, awe wa TAMISEMI au yeyote, akatoa maagizo na kiziwi hajasikia, labda agizo la kutaka eneo fulani wasiwapo watu kuanzia siku fulani, nae kiziwi hajasikia, lazima kesho yake atarudi tena mahali pale. Matokeo yake anaweza kupigwa au kuchukuliwa hatua yoyote kisheria bila yeye kujua," alisema.

Alisema suala la uwapo wataalam wa lugha ya alama kwenye maeneo mbalimbali kama vile hospitali, mahakama na polisi utawasaidia kurahisisha upatikanaji wa huduma pale wanapohitaji.

Pia aliushauri uongozi wa wilaya kuona haja ya kuandaa wataalam wa kutoa elimu ya lugha ya alama kwa muda mfupi kwa viongozi wa serikali ili viziwi wanapofika kwenye ofisi zao wapate huduma inavyostaili.

"Tunaweza kuwa na changamoto inayotukabili lakini tukienda kwa kiongozi yeyote labda mkuu wa wilaya, atatusikiliza, lakini hawezi kujua kwa undani changamoto yetu kama naye hajui lugha ya alama tunayoitumia, hivyo tutakuwa hatujasaidiwa," alisema.

Mmoja wa viziwi, Abasi Kumpuni, alisema ukosefu wa wataalamu hao huwasababishia changamoto mbalimbali ikiwamo kuwa na wasiwasi na kujiona wapweke mbele za watu kwa kukosa wa kumueleza changamoto zao.



Mkurugenzi wa Biashara wa Kampuni ya Halotel, Abdallah Salum (kulia), Mkurugenzi wa Miundombinu wa kampuni hiyo, Justus Kashashari (kushoto), wakishirikiana na mmoja wa waandishi wa habari kufungua shampeni katika hafla ya kuadhimisha miaka sita ya kutoa huduma hapa nchini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbunge alia wananchi kutothaminiwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** MOMBA

MBUNGE wa Momba mkoani Songwe, Condester Sichalwe, amesema wananchi wanavunjika moyo wa kujitolea katika ujenzi wa miradi ya maendeleo inayopelekwa kwenye maeneo yao kwa sababu nguvu zao hazithaminiwi.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Nkana kata Chitete kwenye mkutano wa hadhara ambao uliitishwa kutoa ufafanuzi kuhusu mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Momba unaojengwa eneo la Tindingoma.

Hatua ya kuitishwa mkutano huo ilitokana na malalamiko mengi ya wananchi kwamba viongozi wa kata na Halmashauri ya Wilaya Momba hawajawashirikisha tangu mwanzo katika ujenzi wa mradi huo na badala yake wanatumia mabavu kuwalazimisha kwamba ni lazima washiriki katika ujenzi huo.

"Serikali tujifunze katika hili. Kumekuwa na tabia wananchi wanajitolea katika ujenzi wa mradi hadi wanamaliza lakini inapokuja kwenye tathmini, nguvu ya wananchi inatanjwa ndogo lakini hela ya serikali ikija mfano Sh. milioni 50 haimalizi. Hii inavunja moyo wananchi kujitolea," alisema.

Sichalwe alisema wananchi wanapojitolea kubeba mawe, kuchota maji ijulikane ni shilingi ngapi nguvu za wananchi zimetumika badala ya hivi sasa ambapo haifanyiki na kusababisha manung'uniko.

Alisema Ofisi ya Rais , Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imekuwa ikisisitiza miradi yote ijengwe kwa kutumia 'force account' ili wananchi nao wapata ajira kwenye miradi hiyo, hivyo kupata fedha kidogo ambazo zitawasaidia kwa ajili kuendesha familia zao.

Sichalwe alisema si kwamba wananchi wa kata ya Chitete wamegoma kujitolea katika ujenzi wa hospitaliti ya wilaya bali tatizo lililopo ni kutoshirikishwa tangu mwanzo kwa kupewa elimu namna gani wanatakiwa kushiriki.

"Miradi inapokuja wananchi washirikishwe watoe maoni yao maana ni miradi yao. Hata serikali inaleta fedha sababu inajua kuna wana-Momba," alisema.

Naye Katibu Tawala Wilaya ya Momba, Mary Joseph, aliwaomba radhi wananchi kutokana na makosa yaliyofanyika mwanzo kwa kutowashirikisha.

"Kama utaratibu ulikosewa mwanzo mimi kwa niaba ya halmashauri mwenyekiti na diwani wa kata tunawaomba radhi. Hapa tulipo tunatakiwa tusonge mbele kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa hospitali ya wilaya," alisema.

Nao wao wananchi waliwashutumu viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba kwa kutumia mabavu katika suala la ujenzi wa hospitali ya wilaya badala ya kutumia busara kuwaelimisha.

"Sisi hatujagoma kujitolea ujenzi wa Hospitali ya Wilaya hatukushirikishwa tangu mwanzo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba yeye badala ya kutuelimisha anatufokea lakini sasa mbunge wetu ametuelimisha vizuri sana," alisema Vickitas Simpasa.

Naye Hosea Chilapilo alisema viongozi wa halmashauri walipofika kijijini hapo mwanzo walikuja kibabe na kutaka kuwalazimisha wananchi kujitolea katika ujenzi wa mradi huo hata kabla hawajapewa elimu.

Serikali imetoa Sh. milioni 900 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya Momba ambayo inajengwa eneo la Tindingoma. Awali kulikuwa na mvutano wa wapi ijengwe huku wananchi na mbunge wakitaka ijengwe katika kijiji cha Makamba lakini ikakataliwa na baadhi ya viongozi wa wilaya.

# Tume umwagiliaji yajipanga kukabili athari za tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji imejipanga kimkakati kupitia Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2018, kukabiliana na athari na madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya kilimo.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa katika maonyesho yanayoendelea kuelekea maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani, na Mhandisi Naomi Mcharo kutoka tume hiyo.

Mhandisi Mcharo alisema mabadiliko ya tabianchi yamesababisha ukame na wakati mwingine mafuriko yanayosababisha madhara katika mashamba na uharibifu wa miundombinu ya umwagiliaji. "Kwa hivyo sisi Tume ya Taifa ya Umwagiliaji tuna mpango kabambe ambao tumeainisha kuanzia miaka 10 mpaka 20 ya kukabiliana na mabadilio ya tabianchi, kwa maana ya kwamba tumepanga kuwa na ujenzi wa mabwawa nchi nzima takribani mabwawa 88, ambayo yapo kimakakati katika maeneo kame," alisema.

Pia alibainisha kuwa mabwawa hayo yatajengwa katika maeneo ambayo yanapata ukame kwa muda mrefu na mvua zenye kuleta madhara.

Alisema maeneo ambayo yatajengwa na yamejengwa mabwawa hayo kama vile katika wilaya ya Kwimba yanasaidia kukabiliana na athari na madhara yatokano na mabadiliko ya tabianchi. Awali, Mhandisi Mcharo alisema fedha zinazoingia katika Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji zinatoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni pamoja na ukodishwaji wa mitambo inayomilikiwa na tume. Fedha hizo zinatumika katika matunzo, matengenezo na ujenzi wa miundombinu katika skimu za kilimo cha umwagiliaji nchini.

Mhandisi mcharo alitolea mfano wa ukarabati wa skimu za Pawaga na Dakawa unaoendelea, Ruaha Mbuyuni ambapo ukarabati wa kingo za Mto Lukosi ulioacha njia umekamilika na Urumwi ujenzi unaendelea wa mfumo shirikishi kwa wananchi yaani force account.

# Vituo vya kuoshea magari vyafungwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VITUO vya kuoshea Magari Manispaa ya Shinyanga (car wash), vimefungwa kwa madai ya kutofuata utaratibu wa serikali kuhusu mipango miji.

Mkurugenzi wa Mansipaa ya Shinyanga, Jomaary Satura, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe kutokana na malalamiko kutoka kwa baadhi ya watu kukosa huduma za kuosha magari yao.

Alisema waliamua kufanya operesheni ya kukagua vituo vyote vya kuoshea magari katika Manispaa ya Shinyanga na kubaini wamiliki wake hawakufauta utararibu wa serikali kwa kupewa vibali na ofisa mipango miji.

Mkurugenzi huyo alisema badala ya kufanya hivyo, watoa huduma hiyo wameingia mikataba na wamiliki wa maeneo kitendo ambacho ni kinyume cha utaratibu, hivyo kulazimika kuvifunga.

"Manispaa ya Shinyanga tuna mpango wa kuutengeneza mji kuwa hadhi ya Jiji, hivyo kutokana na kuwapo kwa vituo vingi vya kuoshea magari holela, bila kupata vibali kutoka halmashauri kwa ofisa mipango miji nikaagiza wavifunge vyote na kufuata utaratibu," alisema Satura.

"Hatuwezi kuwa na mji ambao hauna mpangilio. Manispaa ya Shinyanga ndiyo yenye mamlaka ya upangaji mji, lakini unakuta mfanyabiashara ameingia mkataba na Shirika la Reli (TRC), Wakala wa Barabara (TANROADS) au mtu ana kiwanja chake ana sehemu kwa mbele anawekwa 'car wash'. Hilo hatulitaki bali wafike halmashauri wapewe utaratibu,"aliongeza.

Pia alisema hawajafunga vituo hivyo kwa makusudi kwa sababu wanafahamu vimetoa ajira nyingi kwa vijana bali wanachotaka ni kufuatwa kwa utaratibu wa serikali juu ya mipango miji kwa kupata kibali na kuonyeshwa maeneo sahihi ya shughuli hizo badala ya kuweka kila mahari na kuharibu mji.

Baadhi ya wafanyabiashara ambao wanamiliki vituo hivyo, walilalamika kufungiwa vituo vyao ghafla bila kupewa maelekezo yoyote huku wakipewa siku tano hadi Jumatatu ijayo wawe wameshafika kwenye ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kupewa utaratibu wa serikali.

# Sheikh, Askofu wataka kasi usambazaji wa chanjo Kagera

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

BAADHI ya viongozi wa dini katika Mkoa wa Kagera, wameiomba serikali kupeleka haraka chanjo ya corona katika mkoa huo ili wananchi waendelee kupatiwa huduma hiyo.

Wamesema iwapo chanjo hiyo itacheleweshwa inaweza kusababisha wananchi kutokuwa na mwamko wa kuchanja wakati walikuwa wamekwishahamasika.

Wakizungumza na Nipashe baada ya kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge kuwa dozi zote 45,000 za chanjo ya corona zilipokelewa zimekwisha, viongozi hao wa dini kuna umuhimu wa serikali kuharakisha kupeleka dozi zaidi.

Sheikh wa Mkoa wa Kagera, Haruna Kichwabuta, alisema wananchi mkoani hapa walikwishahamasika kuchanjwa na kwamba endapo chanjo hiyo itachelewa, watasahau tena.

"Serikali isiache watu wakapoa, wakishapoa itawapa kazi kubwa tena kuwachemsha. Kwa hiyo chanjo hii inapaswa kupatikana na kuletwa haraka, ikichelewa inaweza kusababisha watu kusahau na kuifanya serikali kuanza tena kuhamasisha wananchi kuchanjwa wakati walikuwa wamekwishazoea," alisema Sheikh Kichwabuta. Pia aliwataka wananchi kuacha kusikiliza maneno ya mitaani kuwa chanjo hiyo ina madhara na kwamba yeye alichanja na hadi sasa hajapata tatizo lolote.

"Yamesemwa mengi kuhusu hizi chanjo lakini sijaona hata moja kati ya yote yaliyosemwa, hivyo yapuuzwe," alisema.

Naye Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kirutheli Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, Dk. Abedinego Keshomshahara, alishauri serikali kuongeza vituo zaidi vya kutolea chanjo hiyo.

Dk. Keshomshahara alisema chanjo itakapoletwa iwe karibu na wananchi, itaondoa tatizo la baadhi ya watu kutochanjwa kutokana na umbali mrefu.

"Kwa kuwa sasa dozi za kwanza zimekwisha hapa Kagera na bado kuna watu wanahitaji kuchanjwa baada ya hamasa iliyotolewa na serikali kwa kushirikana na wadau wengine, ikiletwa nyingine isambazwe zaidi katika maeneo yote hata vijijini," alisema.

Askofu Kesho mshahara alisema kwa kuwa ugonjwa huo unabadilika na sasa unaweza kuua watu kwa haraka zaidi kuliko mwanzoni, ni muda mwafaka watu kuchanjwa ili kujikinga, na kwamba hata Biblia inatambua umuhimu wa kujikinga na kutibu.

Akitoa taarifa kuhusiana na mgawo wa chanjo uliopokewa mkoani Kagera, Jenerali Mbuge alisema mpango wa kutembea nyumba kwa nyumba kuhamasisha wananchi wachanjwe, umewezesha dozi 45,000 kumalizika.

"Sasa tunasubiri dozi nyingine, serikali na watumishi wetu wa afya tumefanya kazi kubwa ya kutembea nyumba kwa nyumba. Mwitikio ulikuwa mkubwa ndiyo maana kufikia Oktoba 10, dozi zote zilikwisha," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania anayemaliza muda wake, Hisham Hendi (kulia), akimtambulisha Mkurugenzi Mtendaji mpya, Sitholizwe Mdlalose (kushoto), kwa waandishi wa habari, wakati wa mkutano wa kumuaga, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi waombwa kuwapa nafasi wasichana wenye uziwi kujifunza

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAZAZI wa watoto wa kike wenye ulemavu wa kutosikia (viziwi) wameshauriwa kuwapa nafasi watoto wao ili waonyeshe uwezo walionao katika kufanya shughuli za kimaendeleo na kukuza uchumi wao. Katibu wa Chama Cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) Mkoa wa Morogoro, Salumu Ally, alisema jana kuwa wako watoto wa kike wenye ulemavu wa aina hiyo lakini wazazi wamekuwa wakiwazuia kwenda popote ikiwamo kujifunza licha kuwapo kwa karakana ya kujifunzia iliyoko katika ofisi za chama hicho mkoa.

Ally alisema wanawake na wasichana hao hubanwa na wazazi wao ambao hawataki kuwaacha watoke sehemu moja hadi nyingine na kufikia hatua ya kuwa na uwezo wa kujitafutia riziki na kuondokana na utegemezi.

Kwa mujibu wa Ally, chama hicho kimeanzisha karakana ya viziwi ili kujifunza mambo mbalimbali na kuwasaidia katika maendeleo kwenye maisha yao, hivyo akawaomba wazazi kuacha tabia ya kuwazuia watoto wa kike kufika kwenye karakana hiyo kujifunza kwa manufaa yao.

Alisema karakana iliyopo inatoa elimu mbalimbali ikiwamo ufundi seremala na ujasiriamali na kwamba vijana 15 wamepitia karakana hiyo na sasa wanaendesha maisha yao. Mmoja wa vijana hao, Abasi Kumpuni, alishukuru CHAVITA kwa kuweka karakana hiyo ambayo imemsaidia kupata uelewa na kuwa fundi seremala mzuri anayefanya kazi huku akiendesha maisha yake na kuondokana na utegemezi.



# HABARI DODOMA

## Serikali kuimarisha huduma kwa watoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imejizatiti kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma kwa makundi maalum wakiwamo watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, aliyasema hayo jana alipokuwa akipokea magari, samani za ofisi na vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kutoka Mfuko wa Abbott kwa ajili ya matumizi katika makao ya Taifa ya Watoto Kikombo mkoani Dodoma.

Alisema utoaji na upatikanaji wa huduma hizo unaenda sambamba na upatikanaji wa nyenzo za kurahisisha huduma kwa walengwa kama vile vyombo vya usafiri pamoja na vitendea kazi.

"Ninafahamu kwamba Makao ya Watoto Kikombo yamewezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa watoto zikiwamo huduma za michezo, elimu afya, msaada wa kisaikolojia na kijamii na ushauri nasaha," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema kupatikana kwa msaada wa magari mawili kwa ajili ya usafiri wa watoto na watumishi kutaondoa kero zilizokuwepo za watoto kuchelewa kufika shuleni.

"Dawa na vifaa tiba katika zahanati na vifaa vya TEHAMA vitaongeza tija katika kutoa huduma stahiki kwa watoto kama ilivyokusudiwa, hii inakwenda sambamba na dhamira ya wizara na serikali kwa ujumla ya kuhakikisha watoto wanaokumbwa na changamoto ya kupata maeneo ya kuishi wanahudumiwa ipasavyo kwa lengo la kuhakikisha wanapata ulinzi na usalama katika makuzi yao,"alisema.

Aliushukuru Mfuko wa Abbott kwa kutoa magari, samani za ofisi na vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya matumizi katika makao hayo kwa kuwa yataongeza ufanisi katika utendaji kazi wa kila siku.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Abbott, Natalia Lebou, alisema wametoa magari na vifaa hivyo ili kusaidia watoto kupata huduma stahiki.

"Mwaka huu ni mara ya kwanza kufika Kikombo na nimefurahi kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhakikisha wanapanga mipango ya kufikiria mbele kuhusiana na makao hayo ya watoto," alisema.

"Sisi tumefurahi kuwa kwenye ushirikiano na wizara tunajua kuna kazi sana ambayo tunafanya pamoja kupanga mipango na kufikiria mbele na hii kazi ni kubwa na tumeendelea na tutakuwepo kwa miaka ya mbele na pia kusaidia kujenga na kutoa huu msaada kwa watoto," aliongeza.

# Unawaji mkono wapunguza maradhi ya kuhara kwa 15%

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema Mfumo wa Utoaji Taarifa za Afya (HMIS) umeonyesha idadi ya watu wenye magonjwa ya kuhara nchini wanaokwenda kwenye vituo vya afya imepungua kwa asilimia 15.

Aidha, unawaji wa mikono kwa kiwango kikubwa umechangia kupunguza idadi ya watu wenye magonjwa ya kuhara katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Kinga Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Ahmed Makuwani, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akitoa tamko la serikali kuhusu maadhimisho ya Siku ya Unawaji Mikono Duniani.

Alisema mfumo huo unaonyesha idadi ya watu wenye magonjwa ya kuhara imepungua kutoka watu 2,630,795 mwaka 2019 hadi 2,233,332 mwaka 2020.

"Hali hii imetokana na hamasa kubwa na elimu inayoendelea kutolewa dhidi ya UVIKO-19 pamoja na kampeni ya taifa ya usafi wa mazingira yenye kaulimbiu nyumba ni choo," alisema

Pia alisema katika nchi zilizoko kusini ya Jangwa la Sahara, takwimu zinaonyesha kuwa ni asilimia 15 ya watu ndio hunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni.

"Hapa nchini kaya zenye vifaa vya kunawa mikono kwa maji na sabuni zimeongezeka kutoka asilimia 21 mwaka 2019 hadi kufikia asilimia 41.8 Juni, mwaka huu," alisema.

Vilevile alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2019 zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na UNICEF, zinaonyesha kuwa asilimia 60 ya watu duniani sawa na watu watatu kati ya watano hunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni.

Kadhalika alisema serikali inawahimiza wananchi wote kunawa mikono nyakati zote muhimu.

"Taasisi zote vyuo, na vituo vya kutolea huduma za afya zihakikishe zinajenga vifaa vya kudumu vya kunawa mikono vyenye maji tiririka ili kuwezesha wanapopata huduma kutimiza lengo la unawaji mikono," alisema

Hata hivyo, alizielekeza sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kutekeleza utoaji wa huduma wa elimu ya afya kwa jamii kwa kutumia vyombo vya habari vilivyoko katika mikoa na halmashauri.



Ofisa Masoko wa kampuni ya Agricom African Ltd, James Leonard (kulia), akifafanua jambo kwa mkulima Ali Amiri, mkazi wa Dabalo, wilayani Chamwino, alipotembelea maonyesho ya zana za kilimo yaliyoandaliwa na shirika la Jatu kupitia kampeni ya Anza na ekari moja, yanayoendelea kwenye viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mawaziri wapitisha vigezo uasili biashara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Mawaziri wa Afrika wanaosimamia biashara wa eneo huru la biashara Afrika (AfCFTA), limepitisha vigezo mbalimbali vya uasili wa bidhaa huku likitoa miezi mitatu kwa wataalam kukamilisha maeneo mbalimbali ambayo hayajakamilika.

Mawaziri hao wamekubaliana baadhi ya vigezo vya uasili wa bidhaa na kufanya vifikie asilimia 88.1 kutoka asilimia 86.03 ya awali ikiwamo vigezo vya uasili wa bidhaa za maziwa, juisi za matunda na vifaa vya bidhaa za ngozi.

Kikao cha mawaziri hao kilifanyika juzi kwa njia ya mtandao kwenye Ofisi za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki jijini hapa.

Akizungumza kuhusu kikao hicho, Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, alisema mawaziri hao walipitia hatua iliyofikiwa katika masuala mbalimbali yaliyomo kwenye awamu ya kwanza ya majadiliano, ambayo bado hayajakamilika na kufanya uamuzi na kuagiza wataalamu kuhakikisha ndani ya miezi mitatu wanakamilisha ili majadiliano yafanyike kwa asilimia 100.

"Tanzania imeridhia mkataba wa AfCFTA ambao hadi sasa nchi 38 kati ya nchi 55 wanachama wa Umoja wa Afrika zimeridhia. Mkataba huu ulianza kutekelezwa rasmi Mei 30, 2020 na nchi 41 zimewasilisha mapendekezo ya 'tariff offer' kwa ajili ya kuanza kufanya biashara.

"Kati ya nchi hizo, zipo jumuiya za Umoja wa Forodha ambazo ni Jumuiya ya Afrika mashariki (EAC), Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Kati (CEMAC), Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) na Umoja wa Forodha Kusini mwa Afrika (SACU),"alisema.

Prof. Mkumbo alisema Tanzania inatarajia kunufaika na kutumia fursa zote za kibiashara zinazotokana na mkataba huo ikiwamo kupatikana kwa masoko mapya ya mazao ya kilimo yatakayochochea uzalishaji.

Pia alisema kuimarika kwa mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo yanayohusisha wakulima wadogo kama vile alizeti, pamba, karafuu, viungo, matunda na mbogamboga kutokana na kuongezeka kwa soko la bidhaa zitakazozalishwa nchini.

"Kuongezeka kwa uzalishaji na ajira kwa wakulima na wadau wanaohusika katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo, kupatikana kwa soko kubwa la bidhaa na huduma lenye idadi ya watu takriban bilioni 1.2 ukilinganisha na idadi ya watu takriban milioni 522 katika nchi za EAC na SADC, kuongezeka kwa tija na ubora kwa bidhaa na huduma za Tanzania kutokana na kuongeza kwa ushindani na hivyo kupelekea kupungua kwa bei za bidhaa,"alisema.

Alitaja faida zingine za kuridhia mkataba huo ni pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kibiashara sambamba na kuviendeleza viwanda na wajasiriamali kundi la wajasiriamali wodogo sana, wadogo na wa Kati (MSME), upatikanaji wa bidhaa za aina mbalimbali nchini na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje ya nchi kutokana na uwekezaji utakaofanyika nchini.





# Waanika dagaa Unguja wahakikishiwa usalama

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema Serikali ya Zanzibar haitawaondosha wananchi wanaojishughulisha na uanikaji dagaa Fungu Refu, Kaskazini Unguja na badala yake itaanzisha mradi mkubwa wa kisasa wa kuliendeleza eneo hilo ili kutoa tija zaidi kwa wananchi kiuchumi.

Othman aliyasema hayo jana katika ziara yake ya kutembelea maeneo mbalimbali yaliyoharibika kimazingira kutokana na mabadiliko ya tabianchi na shughuli za kibinadamu.

Alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa sera ya uchumi wa bluu unaolenga kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutumia rasilimali za bahari na kwamba shughuli zinazofanyika kwenye eneo hilo ni mnasaba na sera hiyo.

Pia alisema kwa kuzingatia uwezeshwaji wananchi kiuchumi, serikali itawekeza mradi huo katika kipindi kifupi kijacho ili shughuli hizo kufanyika katika mazingira bora na ya kisasa yatakayotoa tija zaidi kwa wananchi kiuchumi na kimaendeleo. Alisema mradi huo ni uwekezaji mkubwa na muhimu na wajasiriamali hao watawezeshwa kutumia mbinu bora na za kisasa ili kusaidia kuongeza thamani ya dagaa wanaonikwa na kupata soko katika nchi mbalimbali.

Uwekezaji huo, alisema pia unalenga kuwawezesha wajasiriamali kuwa na uwezo wa kuchakata na kusarifu dagaa wa mbinu za kisasa na kwa kuzingatia ubora ambao itakuwa ni fursa muhimu kwa wananchi kujiendeleza kiuchumi na kukuza maendeleo yao.

Kuhusu fidia kwa wananchi wanaomiliki eneo hilo, Othman aliwahakikishia kwamba kwa kufuata utaratibu, serikali haitawadhulumu na kila mwenye haki atapatiwa kwa mujibu wa sheria.

Aliwaambia vijana wanaojishughulisha na kazi ya upakiaji wa mchanga huko Donge Kidaazini kwamba serikali inafanya mapitio ya sera na sheria ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuwataka kujikusanya ili iwe rahisi kuandaliwa mazingira bora zaidi ya kuendeleza shughuli zao kwa kuingizwa katika mipango ya serikali.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayub Mahammed Mahmoud, alisema eneo la Fungu Refu limekusanya wananchi wapatao zaidi ya 2,500 na wanaendelea kunufaika na shughuli za ujasiriamali wa uanikaji wa dagaa na kujiendeleza kiuchumi.

Alisema hatua ya serikali inapanga kutayarishwa eneo rasmi la ununuaji na ukaushaji dagaa, kujenga gati ya kupokea vyombo vinavyoleta dagaa na kiwanda cha kusarifu dagaa na samaki.

Hata hivyo, alisema mradi huo unamahitaji ya fedha zisizopungua Sh. bilioni 10 na utakapokamilika unatarajiwa kuongeza ajira.

Katika zira hiyo, Othman pia alitembelea eneo la wanajumuiya wanaojishughulisha na upandaji wa mikoko, Fujoni, Kaskazini B, Mashimo ya Mchanga Donge Kidaazini, Donge Mchangani na hoteli ya ZURI iliyoko Kendwa inayoendesha shughuli zake kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira.

## SMZ kuchukua hadhari majanga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itaendelea kuchukua tahadhari za kuwakinga wananchi wake na majanga mbalimbali kwa kutoa elimu ya kuepuka mazingira hatarishi yanayoweza kusababisha maafa.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema hayo jana katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Maafa Duniani, yaliyofanyika katika ukumbi wa Shekh Idriss Abdulwakil, Kikwajuni jijini Zanzibar.

Hemed alisema katika kuhakikisha azma hiyo inafanikiwa, serikali itaviimarisha vituo vyake vya uokozi vinavyosimamiwa na kikosi cha zimamoto na uokozi pamoja na vituo vya uokozi vinavyosimamiwa na Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) kwa kuvipatia nyenzo za kukabiliana na maafa barani na baharini.

Alisema Zanzibar imekuwa ikikumbwa na majanga tofauti yanayosababisha maafa na kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, nyumba 10,043 ziliathiriwa kutokana na mafuriko ya mwaka jana, watu wanane walifariki dunia na matukio 132 ya moto yaliripotiwa kuanzia Januari hadi Septemba, mwaka huu.

Pia Hemed alisema maafa yatokanayo na ajali yameendelea kuwa changamoto na ajali 56 za barabarani ziliripotiwa kwa kipindi cha Januari hadi Septemba, mwaka huu, huku ajali 109 zikisababisha vifo vya watu 128.

Hemed alilitaja janga la corona kusababisha maafa na kuwa tishio duniani na kwamba kwa Zanzibar wagonjwa 4,345 wamethibitishwa kuwa na ugonjwa huo kwa kipindi cha Aprili hadi Septemba, mwaka huu pamoja na vifo 67.



Mratibu wa Jinsia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ofisi ya Makao Makuu Dodoma, Florence Chaki, akiwasilisha mada kuhusu udhalilishaji, wakati wa mafunzo na majadiliano dhidi ya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto, Mwanakwerekwe Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kamishna aeleza athari za ndoa kuvunjika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Amina Thalib Ali, amesema kuvunjika kwa ndoa husababisha athari kubwa kwa watoto ikiwamo kukosa malezi na makuzi bora.

Amesema majukumu ya malezi huachiwa kinamama pekee jambo ambalo ni vigumu kuzifuatilia nyendo za watoto kutokana na harakati za maisha.

Aliyasema hayo jana katika mafunzo ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika ukumbi wa Malaria Mwanakwerekwe, ambayo yaliwashirikisha viongozi wa dini na waratibu wa kupinga vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto.

Aidha alisema vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto vinazidi kuongezeka jambo ambalo linapoteza nguvu kazi wa taifa la kesho kwa kupoteza ndoto zao.

Kamishna huyo alisema ofisi za tume hiyo ziko wazi kwa yeyote mwenye malalamiko awapelekee iwapo ana kesi ambayo taratibu zake zinachelewechwa.

“Hicho kilio ni chetu sote iwapo kuna kesi iko polisi au kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na hata mahakamani ambayo taratibu zinacheleweshwa haiyendi hairudi na watoaji wa haki wako wamewekwa na wanalipwa kwa kazi hiyo. Hapo kuna haki ya mtu inataka kupotezwa njoo tusaidiane kwenye hili janga usikate tamaa,” alisema.

Naye Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mathew Mwaimu, alisema licha ya jitihada za serikali na wadau mbalimbali, kupiga vita vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia na watoto, kesi 868 ziliripotiwa kutoka Zanzibar jambo ambalo linarejesha nyuma maendeleo ya taifa.

Alisema taarifa za ongezeko la vitendo vya udhalilishaji kwa watoto hususan wa jinsia ya kiume ni kubwa kwa Zanzibar jambo ambalo linaashiria maisha ya watoto kuwa hatarini. Mwenyekiti huyo alisema tume imeona kuna umuhimu mkubwa wa wadau kuongeza jitihada ya kutoa elimu ili kuongeza uelewa wa masuala ya haki za binaadamu na utawala bora kwa makundi mbalimbali ya umma.

Pia alisema viongozi wa dini na wanaharakati wakupinga udhalilishaji waliopata mafunzo hayo ni chachu katika jamii ya kuwaelimisha wengine mifumo sahihi ya kutoa taarifa na kudai haki zao.



**KIBA**

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI OKTOBA 16, 2021



# Rosa Ree, kuvishwa pete nd'o unalia?

"UNAJUA mimi najijua mgumu. Kumbe weee, machozi haya hapa. Mapenzi ni mazuri, yanafurahisha pia. Na pale panapokuwa na upendo kati yenu kuna Mungu. Nina furaha hadi nanenepa. Nina furaha sana."

Ni maneno ya msanii mwimbaji, Rosa Ree. Hii ni baada ya juzi kufanyiwa bonge la 'sapraizi' na mpenzi wake King. Ni la kuvishwa pete ya uchumba.

Sasa karibuni wataoana na Rosa Ree atakuwa mke wa mtu.

Alikuwa akielezea furaha yake, kwani hakutegemea siku hiyo kitendo hicho kitafanyika kwenye hoteli moja kubwa hapa hapa Dar..

"Ilikuwa ni siku yake ya kuzaliwa. Tulikwenda kwenye chakula cha jioni. Mimi na yeye tu. Kulikuwa na maua na mishumaa. Tukaongea, huku tunakula na kunywa. Unajua namjua sana, anaongea, lakini anaweweseka. Hayupo vizuri. Nikajua kuna kitu," alisema msanii huyo halafu akaongeza.

"Nikaona kama anafungua kiatu. Akapiga goti, akanivisha pete, nikasema weee, ndiyo inakuwaga hivi."

Rosa Lee alimtambulisha rasmi King mwezi mmoja uliopita. Na wakati anatambulishwa siku hiyo, jamaa alishasema kuwa anatarajia kumuoa hivi karibuni. Na kwa kuanzia tayari kashamvisha pete.

"Sijawahi kufanyiwa hivi na mwanamume yoyote yule, naonaga kwenye 'muvi' tu, lakini unaona mtu kabisa hapa kweli na siyo maigizo kama ninayoyaona ni raha sana eee. Unajua unaweza kuigiziwa unapendwa lakini hupendwi kweli. Lakini pale ambapo unapenda, halafu unapendwa kweli ni kitu kikubwa sana." Rosa Ree aliendelea kutoa 'ushuhuda' wake.

Nadhani sasa kilichobaki ni ndoa tu kwa wapenzi hawa wapya ambao ndiyo habari ya mjini kwa sasa.

## BASI SAWA

## Roma unapiga jiwe gizani?



MSANII Roma Mkatoliki ambaye kwa sasa yupo nchini Marekani, amemsifu msanii mwenzake Ali Kiba kwa kutoa albamu ya 'One Only King', ambapo mbali na kuwa nyimbo zote 16 ni nzuri, lakini hajasikia maneno yasiyofaa au lugha zisizo na staha.

Roma ambaye ni mwimbaji wa nyimbo za 'hip hop, amesema wasanii wengine wa Bongo Fleva wana kitu cha kujifunza kwenye albamu hiyo.

Akiandika kwenye mtandao wake wa kijamii alisema 'Albamu nzima ya mwana. Miwa 16 zinasikia maneno…"(akayataja), lakini hayaandikiki.

"Wasanii na waimbaji kuna cha kujifunza hapa. Au nisiwapangie maisha?" Aliandika Roma Mkatoliki.

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wadau wa muziki, kuwa baadhi ya wasanii wamekuwa wakiimba nyimbo zenye maneno ambayo huwezi kabisa kutaka kuyasikia mbele ya watu unaowaheshimu au wakwe, watoto na wengineo.

## Kingwendu kolabo Diamond, Harmonize



Hii kali sasa. Msanii wa maigizo ya vichekesho, Kingwendu, ameibuka na kusema kuwa anatamani aimbe nyimbo amshirikishe Diamond Platinumz na Harmonize.

"Diamond niliwahi kumtafuta lakini kwa bahati mbaya ana pilikapilika nyingi, Harmonize niliwahi kumpigia simu lakini hakupokea, labda kwa sababu haijui namba yangu. Nachotaka ni kuimba pamoja. Kila mmoja niimbe naye wimbo mmoja au hata mmoja tu akikubali. Mimi ni mwimbaji na mtunzi. Hata sisi watu wa vichekesho tunaweza kuimba na kuufanya muziki uwe mzuri pia." Anasema Kingwendu mtunzi na mwimbaji wa wimbo wa 'Mapepe'. Pia amepamba nyimbo nyingi ikiwamo wa 'Naenda Kusema' wa Aslay miaka kadhaa nyuma.

Alisema anaendelea na jitihada hizo, ingawa bado ngumu. "Unajua wana ushindani, huenda wanaona kuimba na Kingwendu watajishusha au kunipa ujiko mimi, lakini sijakata tamaa, inawezekana."



## COSOTA yachefukwa Kiba kuhujumiwa

BAADA ya kuonekana albamu mpya ya msanii Ali Kiba ikiuzwa kiholeta mitaani, Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), imekuja juu na kusema itachukua hatua kwa watu wote ambao wanafanya kazi hiyo haramu.

Imebainika kuwa albamu mpya iliyotolewa na msanii huyo maarufu nchini, 'Only One King', inauzwa kiholela mitaani kwa wale waliodurufu CD, pamoja na 'flash', bila makubaliano na mhusika, kitu ambacho ni kinyume na sheria.

Katika tamko lao walilolitoa, COSOTA wamekemea vikali usambazaji wa kazi wa muziki, filamu na kazi zingine zinazolindwa kwa Sheria za Hakimiliki usiozingatia utaratibu.

Ikasema kuwa wamepokea taarifa kutoka kwa mmiliki wa lebo ya Kings Music na msanii wa muziki wa kizazi kipya, Ali Kiba, kupatikana albamu yake ya 'Only One King' katika majukwaa mbalimbali ya mitandao ya kijamii inayosambaza kazi za muziki.

COSOTA inasisitiza kuwa itachukua hatua kali kwa watu watakaobainika kufanya vitendo hivyo bila vibali vya wamiliki.

Ikakumbusha kuwa kudurufu kazi ya msanii na kuuza mitaani bila makubaliano yoyote, ni kosa na kuwataka waache mara moja kwani ni kinyume cha sheria.

## Binti wa Kijiji: Kalitwanga dume bazazi

**Na Adam Fungamwango**

NDIYO maana nchi mbalimbali, ikiwamo Tanzania imeweka sheria kali juu ya wanaume wenye tabia mbaya ya kubaka au kutia mimba wanafunzi. Ni kitendo cha kikatili. Si kwa kumfanyia unyama tu mwanafunzi mwenyewe, lakini hata kugharimu maisha yake ya baadaye na ya walezi waliomsomesha, ambayo walikuwa wakimtarajia aje awe mkombozi wao. Taifa pia lilikuwa linamtegemea kuja kuwa mmoja wa wataalam au kiongozi. Lakini mtu mmoja tu kwa tamaa zake anazima ndoto zote za mwanafunzi, wazazi, walezi na taifa zima. Tanzania kwenye hili haina mzaha. Kifungo chake ni miaka 30.

Hata watengeneza filamu wamekuwa wakitoa elimu kwa njia hiyo kuhusu ubaya wa kitendo hicho. Hebu tuiangalie filamu ya 'Binti wa Kijiji'.

Imeigizwa na wasanii Idd Hamisi, Mwanahamisi Madadi, Majuto Mkole, Sumbuko Posho, Ramadhani Mkole na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha kwenye kijiji cha Mfumbwa kuna kijana mmoja ambaye ana tabia mbaya ya wizi. Huku anaitwa Idd. Kila siku yeye ni kesi za wizi tu. Mpaka sasa chochote kikifanyika kwenye kijiji hicho hata kama siyo yeye, basi ataambiwa yeye.

Kwenye kijiji hicho kuna jamaa anaitwa Juto. Huyu anatokea kumpenda binti mmoja anaitwa Mwanahamisi. Hata hivyo msichana huyo ni mwanafunzi.

Anamwambia jinsi anavyompenda na kumuomba awe mpenzi wake. Binti anakataa katakata, akidai yeye bado anasoma.

Kilichotokea ni kwamba Juto akambaka Mwanahamisi . Dunia haina siri, baadhi ya watu kijiji wakafahamu. Ila tu ushahidi walikuwa hawana. Binti alificha.

Baada ya muda binti akawa mjamzito. Na hakutaka kuitoa. Juto kwa kufahamu hilo likifahamika itakuwa ni hatari kwake, akamteka kwanza Idd.




Halafu akamteka denti Mwanahamisi. Akawapeleka porini na kuwajengea kibanda. Lengo ni kwamba Idd akae amtunze Mwanahamisi na ujauzito wake, ili yeye awe salama kijijini. Alivyofikiria sivyo.

Kupotea kwa binti huyo kulisababisha kijiji cha Mfumbwa kuwaka moto. Vijana wakaingia msituni kumsaka msichana huyo. Walimkuta porini akiwa amefungwa na Idd. Juto aliwaambia wakisogea atawaua wote wawili. Kwa ustadi, Mwanahamisi aliupiga mkono wa Juto kisu kikaanguka chini. Ikampa nafasi Idd kumsukuma na kuanguka. Hapo hapo vijana wakavamia na kumkatama Juto ili kumrudisha kijijini kwa ajili ya kesi ya ya kubaka na kumpa mimba mwanafunzi. Mwanahamisi akawa huru.



## Sababu wasanii wachanga kutotoboa

MSANII Obed Jackson, maarufu kwa jina na kimuziki kama Ominous, ametaja moja ya sababu ya wasanii chipukizi kupata tabu sana kutoboa na kuwa mastaa ni kuiga sauti za wanamuziki ambao wameshakuwa wakubwa, Diamond Platinumz na Ali Kiba.

Akieleza changamoto za wasanii chipukizi wanazozipata kwa sasa, anasema kuwa mbali na hilo kumekuwa na ugumu wa wao watoboa kutokana na mambo mbalimbali, ikiwemo pia ukosefu wa pesa.

"Kila msanii anataka aimbe kama Diamond, anataka aimbe kama Ali Kiba, badala ya kutumia vipaji yao kubuni vitu vipya. Ukiimba kama Dimond, mpenzi wa muziki hawezi kukufuatilia anaona unaiga tu, ila ukiimba kwa sauti yako mwenyewe na ubunifu, watu wanakufuatilia. Kingine ni ukosefu nidhamu, idadi ndogo ya watu wanaotuunga mkono, pamoja na uigaji, umekuwa ukituathiri sana," alisema msanii huyo wa Hip Hop, ambaye pia ni mwanafunzi wa Chuo cha Afya Muhimbili.

Baadhi ya nyimbo alizowahi kutoa ni Wimbo wa 'Kimbelembele', 'Jelous' na 'Tutafanana'.

## MBARAKA, MARIJANI WANGEIMBA CHANJO

**Na Adam Fungamwango**

TANZANIA imeungana na mataifa mengi duniani kuhamasisha watu kupata chanjo cha ugonjwa wa UVIKO-19, unaoisumbua dunia kwa sasa.

Viongozi wamekuwa mara kwa mara wakihamasisha wananchi kwenda kupata chanjo ili kuzuia maambukizo ya ugonjwa huo, huku wenyewe wakiwa mstari wa mbele kupata chanjo.

Wizara ya Afya, Maendeleo wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, nayo imekuwa mstari wa mbele kuwahimiza wananchi kuona umuhimu wa chanjo na kupata, huku vyombo vya habari kama kawaida vikifanya kazi yake ya kuhamasisha.

Kuna tatizo kidogo kwenye muziki wa kizazi kipya kwenye kutunga na kurekodi nyimbo za aina hii, ambazo zingewafanya wananchi wazidi kuhamasika zaidi.

Mpaka sasa kuna nyimbo chache sana. Ninayoijua mimi ni ile ya Mrisho Mpoto. Kama zipo zingine sawa, lakini kuna wasanii maarufu hapa nchini ambao kama wangetunga nyimbo za kuhamasisha kuunga mkono juhudi na zingekuwa maarufu zaidi kwa sababu wana mashabiki wengi.

Hapa nawaachia wasanii wenyewe kama wanaona inafaa watunge nyimbo hizo ili kuonyesha uzalendo, lakini pia Wizara inayohusika inaweza kuwatumia kwa ajili ya kufikisha ujumbe.

Ninavyojua, wakati ule muziki wa dansi ulivyokuwa juu miaka ya 1970 hadi 1990, kungekuwa na nyimbo zaidi ya 10 za chanjo.

Wanamuziki kama Mbaraka Mwinshehe Mwaruka, Hemedi Maneti, Mariraji Rajabu, chanzo isingepita bila kuitungia nyimbo.

Hizi ni baadhi ya nyimbo ambazo zilitungwa na wanamuziki hao kuunga mkono matamko ya viongozi, pamoja na matukio ya wakati huo.

**Mama Chakula Bora-Mbaraka**

Ni wimbo uliokuwa unahamasisha wananchi kuhusu ulaji wa chakula bora. Ni baada ya viongozi kuwataka wananchi kula chakula bora badala ya kujaza tumbo kwa ajili ya afya. Mbaraka aliisaidia Wizara ya Afya kwa wimbo huo, kwa kutaja hata aina ya vyakula vinavyopashwa kuliwa. Hii ilikuwa ni katikati ya miaka ya 1970, akiwa na Morogoro Jazz.

**Magaidi wa Msumbiji-Maneti**

Maneti akiwa na Vijana Jazz, mwishoni mwa miaka ya 1980, alitoa wimbo kuungana na viongozi wa Tanzania kulaani magaidi ya Msumbiji. Na hata ni baada ya kifo cha Rais wa Kwanza, Samora Machel, aliyefariki mwaka 1986 kwa ajali ya ndege nchini Afrika Kusini. Ni wimbo uliowafanya Watanzania wengi kuhamasika na kuwa na moyo wa kizalendo.

**Tuitikie wito wa Rais-Marijani**

Baada ya Rais wa Kwanza Mwalimu Julius Nyerere katikati ya miaka ya 1970, kumtaka kila mtu afanye kazi, Marijani Rajab akiwa na Safari Trippers alitoka na kibao ya 'Tuitikie wito wa Rais'.

Aliyarudia maneno yale yale kwenye wimbo wake.

"Tuitike wito wa Rais anavyotueleza, ni wajibu wa kila mzalendo awe mkulima au mfanyakazi, uzururaji na uvivu ni mwiko, tena ni aibu kwako mzalendo, heshima ya mtu kufanya kazi." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo.

**It Can Dan Done- Ahmed Kipande**



Ni katikati ya miaka ya 1960, Mwalimu Nyerere alipoeleza maendeleo ya miaka mitano baada ya kupata Uhuru. Akaja na msemo wa kingereza, 'It can be done, play your part' ikiwa na maana 'inawezekana, timiza wajibu wako'. Kilwa Jazz Band, chini ya Ahmed Kipande wakatoa wimbo uliokuwa na maneno hayo hayo.

**Kilimo cha Kufa na Kupona-NUTA Jazz**

Viongozi walipohamisha vijiji vya ujamaa, kulima kilimo cha kufa na kupona, bendi hazikuwa nyuma. Nuta Jazz, wakaingia studio na kutoa wimbo wa kuhimiza watu walime, ili kujikinga na baa na njaa.



# Tyga mapenzi si makofi

RAPA mkali wa Marekani, Tyga amekamatwa na kuwekwa mahabusu kutokana na unyanyasaji wa nyumbani

Nyota huyo wa muziki anakabiliwa na kosa hilo baada ya mpenzi wake wa zamani Camaryn Swanson kudai kufanyiwa unyanyasaji akiwa katika uhusiano naye.

Kulingana na mtandao wa PageSix, polisi wa Los Angeles walisema walimkamata rapa mwenye jina la Michael Ray Nguyen-Stevenson mwanzoni mwa wiki akituhumiwa kwa unyanyasaji wa mwanamke.



## Foluke tuambie ukweli

MWIGIZAJI kutoka Nollywood ,Foluke Daramola na mume wake, Olukayode Salako, inadaiwa wametengana.

Uvumi huo ulianza baada ya Salako, kuweka posti katika ukurasa wake wa Facebook akiashiria ndo yake haipo tena.


"Foluke Daramola Salako tulijumuika kitanda kimoja hadi jana, nimevunjika moyo nimejaribu kuweka sawa kwa miaka 10 lakini imeshindikana," amesema

## Helen kumbuka hujafa hujaumbika

MCHEKESHAJI kutoka Nigeria, Helen Paul, amesema ajali ya gari imemsababishia uso wake kuwa na michubuko.

Msanii huyo mwenye elimu ya udaktari, amesema kupitia ukurasa wake wa instagram kuwa michirizi iliyopo usoni inatokana na ajali na sio kuzaliwa nayo.

"Kipindi cha nyuma nilipata ajali ya gari mjini Abuja na kusababisha majeraha kichwani na hata nikitaka kupiga picha lazima nivae miwani ya giza kuficha alama" amesema





## Bendera yamponza msanii Nigeria

MSANII nguli wa filamu za Nigeria, Chiwetalu Agu, ametiwa mbaroni kwa kuvaa vazi lenye bendera ya kikundi kiitwacho Ipob, kinachotaka kujitenga na kuchochea watu kujiunga nacho.

Jeshi la Nigeria limethibitisha kumkamata msanii huyo na kudai kumuweka mahabusu, lakini halijamnyanyasa wala kumtesa, ingawa limesema linaendelea kumhoji. Taarifa zinasema kuwa jeshi linatambua haki za raia wote za kutembea kwa uhuru, kujieleza kama haki yao ya kikatiba, lakini halikubali ukiukaji wa sheria wa mtu binafsi au kikundi cha kuchochea umma kufanya ghasia au kuvunja sheria ya utulivu.


Ipob ni kikundi cha watu ambao ni wazawa na eneo ya Biafra lililopo Kusini Mashariki mwa nchi hiyo.

## Princess usije kuukana ulimi

MWIGIZAJI kutoka Ghana, Princess Shyngle, ambaye anasifika kwa kuwa na umbo matata, amesema anaweza kujiondoa katika mitandao ya kijamii kama mpenzi wake akionyesha kutopenda jambo hilo.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, mrembo huyo amesema hakuna mtu atakayemtoa katika matumizi ya mitandao, isipokuwa mpenzi wake pekee.

"Kama nikimwona mpenzi wangu hana raha kuhusu matumizi yangu ya mitandao, hakika nitafuta akaunti zangu zote," amesema



MAKALA

# Utomvu wa miti, utajiri wa bure uliojificha bado wengi hawaujui

## •Prof. SUA: Ukichoma miti, unachoma noti

Na Felix Mwakyembe, MBEYA

KUNA maelezo, jamii zilizopo kwenye maeneo yenye ukame hazinufaiki sana na kilimo, hata hivyo kuna neema iliyojificha utomvu, fursa ya kiuchumi inayopatikana kwa wingi katika maeneo ambayo hayajapewa umuhimu unayostahili.

Utomvu ni zao misitu lenye thamani ukifahamika zaidi kwa majina ya kitaalamu, "gums and resins," ikitegemea aina ya mti unaozalisha,

Mchambuzi wa Sera za Umma na Uwekezaji Misitu na Usimamizi wa Maliasili, Robison Ng'ethe kutoka Kenya, anasema mazao hayo ya utomvu yako aina mbili, ambayo ni kimazingira na kiuchumi.

Wataalamu wa misitu wanauelezea umuhimu wa utomvu kwa mazingira, ni pamoja na kupunguza utegemezi wa binadamu kwa misitu ya asili, kukidhi mahitaji yao ya msingi kama nishati, kwa kukata kuni na mkaa, mbao na miti ya ujenzi na magogo.

Ni wazi, iwapo wananchi watajishughulisha na biashara ya upandaji miti itakayowaingizia fedha na wakati huohuo kuwapatia mahitaji ya msingi, itapunguza utegemezi kwenye misitu ya asili ambayo ni muhimu kwa mazingira.

Ugemaji utomvu kutoka kwenye miti ya asili (acacia) inayopatikana kwenye maeneo ya ukame, inaepusha ukataji miti, kwa kuwa inawapatia fedha kutoka mazao hayo.



Ugemaji utomvu ukiendelea. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### PANAKONUFAIKA

Mikoa inayotajwa kuswa fursa ya biashara ya utomvu, hususani aina ya "gums," ni pamoja na Singida, Shinyanga, Tabora, Dodoma, Morogoro, Manyara, Kilimanjaro na Geita. Panakoathiriwa na ukame, pia ndiko kunakopatikana zaidi miti ya asili aina ya acacia.

Uhifadhi misitu unatajwa kuwa muhimu zaidi kwa ustawi wa binadamu, kwani ndiko penye vyanzo vya maji, hutoa nishati (kuni na mkaa), mbao, dawa, utalii, makazi kwa viumbe hai na mazalia ya samaki.

Miongoni mwa miti inayotumika kugema utomvu aina ya 'gum,' ni ya asili na aina ya 'resins' unagemwa kutoka kwenye miti ya kupandwa, aina ya misindago (pines).

Uwekezaji kwenye miti hiyo ya misindago hunufaisha kupitia uvunaji gundi aina ya 'resins' kwa miaka isiyopungua mitano katika kipindi cha miaka 18 ambacho cha kusubiri uvunaji mbao.

Wananchi waishio kwenye maeneo yenye ukame, hunufaika na miti ya asili iliyopo kwenye eneo lao, kazi yao ni kuilinda na kuitunza hiyo misitu ili kugema gundi aina ya 'gum' itakayowaingizia fedha.

Utomvu aina ya 'gums' na 'resins' hutumika kuzalisha dawa mbali mbali kwa ajili ya mbao (varnish), rangi za nyumba, dawa za karatasi, rangi zinazotumika kuchanganyia kwenye rangi (tinnier), manukato, chuinghum, vyakula na kwenye mipira ya magari, pikipiki na baiskeli.

### THAMANI YA BIDHAA

Fursa hizo za kiuchumi, zinamfanya Rasi wa Ndaki ya Misitu, Wanyamapori na Utalii, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Prof. Suzan Augustino, Analinganisha uchomaji miti, ni sawa na kuteketeza fedha, akikielezea akitumia maneno mawili 'usichome noti!'

Hesabu kutoka kwa watalamu misitu iliyopo ni kwamba, mita moja ya mraba wenye ujazo kwa mti wa msingano (pine) inakadiriwa kuzalisha mbao zenye thamani ya Sh. 80,000 unapofikia umri wa kuvunwa.

Pia anasema katika mazingira hayo, wakati haijatumika, inazalisha utomvu kwa uwezo wa kuingiza zaidi ya ferdha Sh. 25,000 kila miaka mitano. Kwa mantiki hiyo, mti mmoja una uwezo wa kuzalisha zaidi ya Sh. 100,000 katika uhai wake.

Wataalamu wanashauri muda wa ugemaji ni kati ya miaka mitano hadi nane, kutegemea ubora wa mti. Wastani ni kila mti hutoa nusu kilo ya utomvu kwa mwezi, ambayo ni sawa na kilo sita kwa mwaka na kwa bei ya serikali kilo moja huuzwa Sh. 855.



Mtaalamu akionyesha shughuli za ugemaji utomvu wa miti.

### OFISA UHIFADHI

Lipo tatizo la kupitiliza katika ugemaji, hivyo kuathiri ustawi wa mti na Ofisa Uhifadhi Mkuu, Wakala wa Huduma za Misitu nchini, Salehe Beleko analifafanua:

"Hivi sasa unaandaliwa mwongozo utakaosaidia wakulima na wadau wengine wenye kugema utomvu ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza kwenye miti inayogemwa."

Beleko anaeleza kuwapo mpango wa kuanzisha mashamba mahsusi kwa ajili ya uvunaji utomvu, kama lengo la msingi na mbao ikibaki kama faida tu, hatua anayoielezea itapunguza kama sio kuondoa, tatizo la watu kutegemea misitu ya asili.

Mazao jamii ya utomvu inayogemwa kutoka kwenye miti, yanatajwa na wanasayansi ya misitu kuwa yanatoa fursa nzuri zaidi za kiuchumi kwa kuboresha maisha vijijini na kupunguza umasikini kwenye jamii.

### MNYORORO THAMANI

Kwenye mnyororo wa wadau wa biashara ya utomvu, unagawanyika kwa: Wazalishaji au wakusanyaji (96.5%); wachuuzi (3%); wafanyabiashara (0.5%); na wasafirishaji nje ya nchi (0.14%).

Watafiti wanayaelezea mazao hayo kuwa na thamani za kijamii, kitamaduni, dawa, kazi za kimazingira na kuchangia mapato kwenye serikali za mitaa na serikali kuu.

"Pamoja na manufaa yake yote hayo, kiwango cha uzalishaji gundi Tanzania kipo chini sana," anabainisha Prof. Boniface Mbilinyi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine.

Ni hivi karibuni. Prof. Mbilinyi amewasilisha andiko lake kuhusu hali ya uzalishaji na biashara ya utomvu nchini, katika 'Mkutano kwa Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris na Namna Jamii Zinavyohimili Mabadiliko ya Tabianchi' ulioandaliwa na Jukwaa la Misitu Afrika (AFF) na kuendeshwa kwa njia ya mtandao ukiunganisha nchi nne za Kiafrika.

Prof. Mbilinyi anasema anatumia takwimu za uzalishaji kwa aina zote mbili 'gums' na 'resims' kuanzia mwaka 2005 hadi 2019, kuthibitisha kuporomoka uzalishaji wa mazao hayo nchini.

Mwaka 2005 Tanzania ilizalisha tani 1,169, ukashuka hadi tani 965 mwaka 2006, kabla ya kupanda kufikia kiwango cha juu zaidi ambacho hakijafikiwa tena cha tani 1,174 mwaka uliofuata.

Mwaka 2007, mwenendo wa uzalishaji mazao hayo ukaanza kuporomoka hadi kufika tani 755 mwaka 2019, haki inayohusishwa na kukosekana tathmini ya msingi kwa rasilimali hizo na uelewa kuhusu umuhimu wa mazao hayo.

Prof. Mbilinyi anashauri kufanyika kwa tathmini ya rasilimali hizo, kupata taarifa mpya ya kusambaa uzalishaji wake nchini, pia akitaja kuwapo tatizo la kukosekana viwanda vya kuchakata utomvu huo, kwa ajili ya kuongezea thamani.

Mtazamo wa kitaalamu wa msomi huyo ni kwamba, Tanzania iendelee kuwa mzalishaji na msafirishaji wa malighafi hiyo ya utomvu nje ya nchi na waagizaji ni vyema wakahitaji bidhaa zake kutoka viwandani vya nchii.

Wataalamu wanashauri kupitiwa upya kwa sera zote zinazohusika na mazao hayo wakibainisha kuwa sera rafiki zitaongeza thamani ya mazao hayo ya utomvu na hatimaye kuongeza, pia uzalishaji.

Kenya ni miongoni mwa wazalishaji na wasafirishaji wakubwa wa utomvu barani Afrika, wakishika nafasi ya tatu baada ya Ethiopia na Somalia.

Uwezo wa uzalishaji aina zote za utomvu unakadiriwa kuwa zaidi ya tani 26,000 kwa mwaka, sehemu kubwa ikiuzwa nje ya nchi kama malighafi, na kiasi kidogo kinachobakia huchakatwa kwenye viwanda vichache vilivyomo katika nchi hiyo.

# Wenye msitu wapigana kutetea bei ya mkaa, bidhaa zinazoendana nazo

**Na Christina Haule,** MOROGORO

TANGU zama zilizopita kumekuwapo usemi 'misitu ni uhai.' Ni kweli inaendelea kuenziwa na kuna hatua ya kimamlamka ya utendaji inayoitwa Usimamizi wa Shirikishi wa Mazao Misitu (USM).

Mti ni mzizi unaotajwa unamudu kuzaa matunda kwa wananchi kitaifa kwa ujumla, iwapo watashirikishwa mapema katika yanayowahusu katika eneo hilo.

Mratibu wa Kikundi Kazi cha Misitu Tanzania (Tanzania Forestry Working Group (TFWG), Casian Sianga, anasema sheria za misitu na sera zake, ikiwamo ya mwaka 1968, imeweka wazi uhifadhi na usimamizi wake endelevu kwa ajili ya vizazi.

Anasema ushirikishaji duni wa serikali za vijiji umechangia wavunaji mazao, wanahofu utekelezaji, hawapati mapato stahiki ya kuwakwamua kiuchumi, serikali kuu na wilaya zake, kwani hawanufaishwi na mapato ya misitu vijijini mwao.

Sianga anasema, wamechunguza na kubaini faida na shida wanazopata wavunaji mazao ya misitu, baada ya kupewa elimu na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), kupitia Usimamizi Shirikishi wa Misitu Jamii (USMJ).

Anachanganua, wilaya ya Morogoro ilianza kuvuna mazao misitu kwa njia endelevu mwaka 2017, katika vijiji 157 vilivyotembelewa, kumekuwapo jumla ya makusanyo Sh. 80,521,300.

Anasema wilaya Kilosa iliyoanza uvunaji endelevu wa mazao misitu mwaka 2013 hadi 2021 walipotembelewa na kuchunguza makusanyo yao, walionyesha jumla ya Sh. mil 56,899,300 kwa vijiji 149.

Sianga anasema ni jambo linalokuwa sawa pasipo mabadiliko, hata matamko ya serikali za vijiji kwa asilimia 90 vingefanya usimamizi shirikishi na biashara endelevu na kuweza kukusanya kiasi cha Sh. bil 4,172,000,000 kwa Kilosa na Sh. 4,446,000,000 kwa Morogoro.

Anasema upotevu wa fedha umetokana na mgongano wa maelekezo ya bei za mauzo baina ya serikali kupitia mwongozo waliotoa mwaka 2019 na wavunaji mazao ya misitu, kupitia sheria walizoziweka na kufanya makusanyo kuyumba kuanzia kipindi cha mwaka 2004, 2017 na 2019.

**SHAKA LA TAMKO**

Suianga anafafanua, kuna wakati matamko ya kijamii, huchangia kushuka mapato katika wilaya zao, akiwa na ufafanuzi, wilayani Morogoro kuna vijiji vilivyoathirika katika uvunaji endelevu wa mazao, misitu na migawo ya pesa.

Kimsingi, mgawo wa halmashauri unatakiwa kupata asilimia 10 ya mapato yote, kamati za mazingira asilimia 30; na halmashauri ya kijiji asilimia 60 kwa ajili ya miradi yake ya maendeleo, kama vile ujenzi wa shule, hospitali, zahanati na kuajiri walimu wa muda.



**SHDA VIKWAZO**

Ofisa wa Kujenga Uwezo kutoka TFCG, Simon Lugazo, anasema wamechunguza katika vijiji tisa vya Kilosa na Morogoro, kutaka kujua vikwazo kwa uvunaji endelevu wa mazao misitu, wakiwasiliana na watoa uamuzi wa miongozo na sera, ili waisaidie jamii tajwa.

Anavitaja vijiji walivyotembelea ni Matuli, Lulongwe, Diguzi, na Mlilingwa wilayani Morogoro, huku Kilosa kuna vijiji vya Ulaya Mbuyuni, Chabima, Kitunduweta, Ihombwe na Msimba.

Anasema mwaka 2019 kulikuwapo tamko linaloelekeza bei za mazao ya misitu, ikitaka jamii kuuza gunia moja la mkaa kwa bei ya Sh. 12,500 wakati zamani wavunaji waliuza kulingana na upatikanaji wa wateja wao.

"Lengo la vijiji kuweka mpango wa kupanga bei zenyewe ni kutokana na kutafuta namna ya kuvutia wateja. Bei hiyo ni changamoto kwao," anasema na kuongeza:

"Sababu ya maeneo waliopo na wengine, wamekuwa wakipunguza bei ili kuleta ushawishi kwa wateja kuweza kufika kununua bidhaa. Yapo maeneo vijijini tumeshindwa hata kwenda na gari, lazima upande pikipiki."

Anafafanua kuwekwa bei ya pamoja, kumechangia mavuno na mapato ya mazao misitu kupungua kwa kiasi kubwa, hata kuleta sintofahamu kwa wavunaji.

Kunatajwa kiulizo kama watakosa kipato kutokana na zuio hilo la sokoni, namna gani watamudu kuhifadhi misitu, kwa sababu wanatumia fedha.

Lugazo anasema, walipoanza usimamizi shirikishi, kulikuwapo fursa kwa wananchi kupanga bei kulingana na hali halisi, ili kumvutia mteja afikie katika maeneo yao.

Anasema kwa sasa wanakwamishwa na bei elekezi ya mauzo, Sh. 12,500, ilhali awali walikuwapo wateja waliowafikia kwa sababu bei chini, mfano hai ni Sh. 5000 kwenye maeneo yasiyofikika kirahisi.

Anafafanua:"Ikumbukwe kwamba, wananchi wenyewe ndio wameamua watunze eneo la msitu na kama itaonekana hakuna faida, inaweza kuleta changamto baadae na hivyo kupunguza morali kwao kuendelea na shughuli za misitu, kwa wao kutoona faida za misitu."

Lugazo anasema, hivi sasa wamejipanga kutangaza kwenye gazeti la serikali kuhusu misitu iliyotengwa na vijiji kwa ajili ya uhifadhi, kuwezesha kama wananchi watataka kubadilisha matumizi, kuwapo hatua zake.

Anasema lengo la TFCG ni kuongeza idadi ya vijiji vya uhifadhi katika mradi ya hifadhi misitu, kupitia usimamizi endelevu wa misitu wa biashara nchini, pia kushawishi watoa uamuzi na waunda sera na miongozo, wafanye mabadiliko yatakayosaidia wananchi

Hadi mwaka 2019, anasema wameshaongeza wilaya zenye mradi ambazo ni: Ruangwa, Liwale na Nachingwea mkoani Lindi; na Iringa iko Kilolo, huku mkoa Morogoro zipo wilaya Mvomero, Kilosa na Morogoro.

Pia yahusuyo kupanda na kushuka mapato ya mkaa, mwanakijiji Chala Kauzeka, anayeshughulikia mazao misitu kutoka kijiji cha Ulaya Mbuyuni, anakiri udhaifu wa kitaalamu katika uzalishaji mazao misitu.

Anashauri serikali ingewapa nafasi ya kuzungumza, ili kufahamu shida iliyoko katika gharama za ushuru na ununuzi wa bidhaa misitu sasa.

**WADAU MISITU**

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Charles Meshack, ana ufafanizi kuwa mkaa unachangia Pato la Taifa kwa asilimia 1.3, huku sekta nzima ya misitu ikichangia kati ya asilimia 2.7 na tisa.

Anasema, sehemu kubwa ya pato hilo linachangiwa na mkaa, ingawa kuna angalizo la upande wa pili wa shilingi, tahadhari ya sehemu kubwa ya mkaa kuvunwa kiholela, hata kuhatarisha upoteaji misitu mingi, ikibashiriwa balaa linalonyemelea kati ya miaka 20 na 40 ijayo.

Meshack anashauri haja ya sekta mkaa, ikarasimishwa rasmi iwe sehemu ya sera na mfumo wa kisheria wa kutambua mchango wake kiuchumi na mpango wa viwanda kwa jamii.

Anaeleza uzalishaji mkaa ni suala mtambuka, linalogusa sekta mbalimbali kama vile, kilimo, nishati, misitu na ardhi na kuna wakati hupatikana mkanganyo unaochangia sekta hizo kugongana.

Mkurugenzi hiyo ana mtazamo wa haja ya sekta hizo zikae pamoja kuwezesha mkaa ujavunwa kwa namna uendelevu yenye faida kwa jamii na Taifa.

Mkufunzi Mwandamizi wa Habari za Mazingira, Deodatus Mfugale, ana maoni kwamba msitu unapaswa kutunzwa vyema na kuingiza katika dhana halisi ya 'kiwanda katika msitu' iliyopo sasa.

Kimsingi, anasema fedha za mauzo ya mazao misitu, huingia kwenye mnyororo wa thamani kuanzia uandaaji eneo la uvunaji hadi mauzo na kufanya wanakijiji wa eneo husika wanufaike, hata kama hawahusiki na uvunaji wake.



Sehemu ya shughuli za mkaa endelevu kwenye magunia, kijiji cha Ulaya Mbuyuni wilayani Kilosa. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**

HABARI KIMATAIFA

# Kenyatta akutana na Biden

**WASHINGTON D.C,** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, wamejadili uwazi wa kifedha katika mkutano wao juzi katika Ikulu ya Marekani, wakati kiongozi huyo kutoka Afrika Mashariki akikabiliwa na uchunguzi kuhusu taarifa kuwa yeye na familia yake wameficha mamilioni ya dola katika akaunti za siri ughaibuni.

White House ilisema viongozi hao wawili walisisitiza umuhimu wa kuongeza uwazi na uwajibikaji katika mifumo ya kifedha ya ndani na nje ya nchi.

Kenyatta ni mmoja wa zaidi ya wanasiasa 330 wa sasa na wa zamani waliotambuliwa kuwa warithi wa akaunti za siri zilizofichuliwa katika ripoti za karibuni zinazofahamika kama Nyaraka za Pandora.

Katika mkutano huo, Biden alitangaza ushirikiano katika vita dhidi ya janga la corona.

Biden na Kenyatta waliahidiana kufanya kazi pamoja kuhusu mabadiliko ya tabianchi na kumaliza machafuko katika pembe ya Afrika.

**DW**



Rais wa Marekani, Joe Biden, amekutana na kufanya mazungumzo na mwenzake wa Kenya, Uhuru Kenyatta katika Ikulu ya white house, nchini Marekani. **PICHA RFI**

# Lebanon yaomboleza baada ya vurugu za kimadhehebu

**BEIRUT,** LEBANON

LEBANON jana iliwazika wahanga wa machafuko mabaya ya kimadhehebu kuwahi kushuhudiwa kwa miaka mingi, baada ya milio ya risasi kurindima katikati ya mji mkuu Beirut kwa saa kadhaa juzi na kurejesha kumbukumbu ya vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Watu sita waliuawa na wengine kadhaa kujeruhiwa wakati vurugu zilipozuka kufuatia mkutano wa waandamanaji wa Kishia wanaodai kuondolewa kwa Jaji anayechunguza mlipuko mkubwa wa mwaka jana katika bandari ya Beirut.

Vuguvugu ya Kishia ya Amal na Hezbollah ambayo yaliandaa maandamano hayo yalikituhumu chama cha Kikristo cha Lebanese Forces kwa kuanzisha vurugu kwa kuwashambulia waandamanaji wakiwatumia walenga shabaha.

Wakati mipango ya mazishi ikiendelea jana Kusini mwa Lebanon na mji mkuu Beirut, nchi hiyo imefanya maombolezo ya kitaifa yaliyotangazwa na ofisi ya rais.

Ufaransa, Marekani, Umoja wa Mataifa na Iran zimeomba utulivu lakini pia zikasisitiza kuhusu haja ya kuruhusu uchunguzi wa mripuko wa bandari kuendelea bila vikwazo.

**DW**

# Poland yapitisha sheria inayoruhusu wahamiaji kuzuiwa mpakani

**WARSAW,** POLAND

BUNGE la Poland limepitisha marekebisho ya sheria yanayoruhusu wahamiaji kuzuiwa mpakani na maombi ya hifadhi kutoka kwa wahamiaji waliongia nchini humo kinyume cha sheria yapuuzwe.

Wabunge pia waliridhia mpango wa serikali kujenga ukuta kuwazuia wahamiaji wanaovuka kutoka Belarus, mradi ambao unakaridiwa kugharimu Euro milioni 353.

Haya yanajiri wakati katika miezi ya hivi karibuni, maelfu ya wahamiaji wengi kutoka Mashariki ya Kati wamekuwa wakijaribu kutoka Belarus kuingia Poland au Latvia na Lithuania.

Mashirika ya kutetea haki za binadamu, tayari yameishutumu Poland kwa kuwazuia wahamiaji mpakani na kuwalazimisha kurudi Belarus.

Chini ya sheria mpya iliyorekebishwa, raia wa kigeni atakayezuiwa baada ya kuvuka mpaka wa Poland kinyume cha sheria atahitajika kuondoka mipaka ya Poland na atapigwa marufuku kuingia nchini humo kwa kipindi cha kati ya miezi sita hadi miaka mitatu.

**DW**

# Wanajeshi wa zamani wa Afrika Kusini wawateka mawaziri

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

MAWAZIRI wawili na Naibu Waziri wa nchini Afrika Kusini, wameokolewa baada ya kutekwa na wanajeshi wa zamani walioshiriki katika vita ya kupinga utawala wa watu weupe wachache.

Wanajeshi hao wa zamani wanataka kulipwa fidia kwa jukumu walilolifanya.

Wanajeshi wa zamani wa vita vya ukombozi kutoka upande wa ANC wanataka kulipwa kiasi cha fedha cha $280,000 (£203,000) kwa ajili ya makazi na bima ya afya kwa ajili ya familia zao.

Walikutana na waziri katika ofisi ya rais Mondli Gungubele, Waziri wa ulinzi, Thandi Modise na Naibu wake, Thabang Makwetla, kujadiliana kile wanachokitaka katika hoteli iliyopo mjini Pretoria, usiku wa juzi.

Maofisa wa serikali walitekwa baada ya majadiliano hayo kushindwa kufanyika. Baadaye zaidi ya watu 50 walikamatwa baada ya majaribio ya kujadiliana juu ya kutolewa kwa mateka kutofaulu.

Kikosi maalum ambacho wajumbe wake wanavaa sare za kijeshi na wamepata mafunzo ya kukabiliana na utekaji, walipaswa kuitwa, Gungubele alisema tukio halikubaliki kisheria.

Awali wanajeshi hawa wa zamani walisema wanahisi chama cha ANC kiliwasaliti kwasababu hawakuwahi kulipwa fidia kwa kushiriki mapambano dhidi ya serikali ya ubaguzi.

Hata hivyo wanajeshi hao wanalipwa pensheni ya kila mwezi. Mapema wiki hii kundi hilo lilizunguka nje ya ofisi za ANC.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

TAJIRIKA FUGA MAJOGOO WA KIENYEJI WEUPE WA NYAMA WAITWAO BOVANS TOKA PARANGU FARM WANAOHIMILI MARADHI NA WANAOVUNWA HARAKA UPIGE PESA. VIFARANGA WAPO WA SIKU HADI MWEZI MMOJA KWA ODA.

**TUPIGIE: 0673 722 823**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MAOMBI NO. 53 YA 2021**
**GODWIN MUSHI……………….............................MDAI**
**DHIDI YA**
**FELISTER ARON KALINGA……….................……..MDAIWA**

**KWA: FELISTER ARON KALINGA**
**KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa mleta maombi ameleta maombi yake ambayo maelezo ya maombi yake yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria Mahakama hii binafsi, Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya Jumanne, tarehe 19 Mwezi wa 10 Mwaka 2021 saa 2:30 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

**ANGALIZO:**
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 27 Mwezi wa 09 Mwaka 2021.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARY STAIL MPUTA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3655-0014** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **NYASA mwaka 2014**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochite cha polisi

Polisi taarifa
DAR/CHA/RB/427031/2020

---

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**IBRAHIMU BURHANI KAMARA** anatangaza kupotelewa na result slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.4183/0319** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **BINTI MUSA** mwaka 2020,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa
DAR/BUG/RB/494850/2021

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**Swabrina Idris Kassim** amepotelewa na cheti cha chuo chenye registration namba **943** kilichotolewa na Chuo Kikuu cha **Hubert Kairuki mwaka 2018** ,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi taarifa DAR/MAG/RB/ 400012/2021

---

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

**JOYCE WILLIAM SANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 569 BTZ – Isuzu Journey.** Chassis **Na. BE287100116.** Engine **Na. 4BG1254123.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 673 BEZ** – Nissan Civilian. Chassis Na. **RGW40001285**. Engine N**a. TD42033066.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DSM/PHQ/ RB/472817/2021.

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**CIVIL CASE NO.11 OF 2021**
**FLORENT KYOMBO and**
**FRANCISCA KYOMBO……………….………… PLAINTIFFS**
**VERSUS**
**ANDREW ALOYCE……………………..…...... DEFENDANT**
**NOTICE OF EX-PARTE JUDGEMENT:**

**To: ANDREW ALOYCE**

**YOU ARE HEREBY NOTIFIED** that the court has fixed to pronounce its judgement with regard to the above mentioned case.

**TAKE FURTHER NOTICE** that the judgement will be pronounced in open court before Hon MPEMBELWA RM Magistrate on the 22nd day of October,2021 at 8:30am o'clock in the forenoon/afternoon

**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT THIS 12 day of October,2021.**

MAGISTRATE

---

**Magistrates Court( Approved Forms For the Primary Court)**
**GN. NO 943(Contd.)**
**FOMU MADAI -3**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha URU Mkoa Kilimanjaro**
**Shauri la Ndoa Na 02, 2021**

**Jina la Mdai SIMON ANTHON CHUWA**
**Jina la Mdaiwa EMILIANA ERNEST NZWALILA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

*(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)*

**Kwa: EMILIANA ERNEST NZWALILA**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yake /yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai )

**Madai ya talaka dhidi yako**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 18 mwezi 10 mwaka 2021 saa 03:00 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 4 mwezi 10 mawaka 2021

…………………………………………
**HAKIMU**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATEI FRANCIS MKANTA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUBARU LEGACY** yenye namba za usajili **T 839 DGT** chasis namba **BL5015090** enmgine namba **E520C075213,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **DAR/URA/ RB/495730/2021**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

ISACK S KIDUTA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 907 CTN KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KAH/RB/510/2021

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

KITANUKE BARAKA NDITIYE ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC186 BZH KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KIG/ KAK/RB/ 463604/2021

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
Katika mahakama ya mwanzo MJINI TANGA
Usimamizi wa mirathi 172/2021

Ombi la **FATUMA SALIMU ALLY** kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **HALIMA FENI CHUPA**

KWA.YEYOTE ANAYEHUSIKA
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhjuria kesi wakitaka mnamo tarehe 22/10/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mkirathi hiyo
Wosia wa mareheumu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOHN AMON SANGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T.892 DLW. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI SON/TUN/ RB/764303/2020

---






**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake amekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka Mke Wangu-15

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Unajua mimi siku hizi natembea kwa tahadhari sana, kwa hiyo naomba tu kama unaweza njoo nyumbani kwetu hapa Msangani."

"Haina neno shoga nitakuja kukupatia ujumbe wako."

"Haya, mchana mwema."

"Nawe pia."

Alitaka simu. Akamtazama Tom.

"Tom, najua hupendi ninavyotaka kufanya, lakini naomba tufanye hivi kwa sababu tunaweza kupata kitu kingine ambacho hatukitarajia."

"Nimekwambia kwa sababu ni wewe basi mimi nitafanya kila unachotaka."

"Sasa ni hivi. Mimi nakwenda hadi huko. Halafu wewe uwe nyuma yangu. Ni kwamba nitakapokuwa naongea naye mimi nitapiga simu kwenye namba yako, na wewe utakuwa unasikia maongezi yetu. Utasikua kila kitu na baada ya muda na wewe uje hapo hapo."

Ni kama vile Tom alianza kumuelewa Tedi. Nadhani alichotaka ni Farida kukiri kila kitu mbele yake na yeye anasikia, ili kama msamaha kutoka uwe pale na kama talaka na kuachana taratibu zianzie hapo hapo. Alimtazama na kumsifu kimoyomoyo kuwa ni mwanamke mwenye akili.

"Wazo zuri mpenzi, kama vile nimeanza kukuelewa, lakini bado kidogo."

Tedi alicheka kicheko cha mbwembwe za kike. "Unanielewa tu mwaka huu."

Kwa mara ya kwanza tangu kupambazuke, Tom aliangua kicheko.

************************

"Lakini mbona mimi sikujui?"

"Mimi nakufahamu si ulikuwa unaishi Kigamboni Kibada. Nadhani utakuwa umenisahau na huwezi kukumbuka wote kwa sababu hatukuwa mashoga, ila mimi nilikuwa nakuona tu unapita kwetu. Mimi naishi kwenye duka na Malembeka."

Tedi alidanganya. Na hata jinsi ya kudanganya hivyo alipata kutoka kwa Tom. Yeye ndiye aliyempa ujanja huo akifika nyumbani kwa kila Farida aseme vipi ili aaminiwe kuwa ni kweli ametoka Kigamboni na anamfahamu.

Kwa maneno yale tu, Farida aliamini. Alimuamini kwa sababu ni kweli ilikuwa si rahisi kuwajua watu wote Kigamboni. Hasa ikizingatiwa kuwa hakuwa mzaliwa wa kule, au kuishi kwa muda mrefu. Ni kwamba alikwenda pale kwa dada yake akitokea Morogoro kumkimbia Sam. Aliishi kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja, ndipo alipokutana na Tom, maeneo ya Kariakoo na kuunda urafiki, mapenzi, hadi ndoa.




"Nashukuru sana. Ila shoga yangu mimi sitoandika chochote. Nitakwambia tu nenda kwamwambie atafute mke mwingine aoe, mimi sikuwa chaguo sahihi kwake."

Na ni kweli alilifahamu dula la Malembeka ambalo ni maarufu sana maeneo yale. Isingekuwa rahisi kwa mtu ambaye hapajui Kigamboni kufahamu duka hilo.

"Enhee, amekupa ujumbe gani?"

Tedi alichukua mkoba wake na kutoa karatasi akampatia.

"Basi mimi naomba niondoke."

"Hapana. Nataka nisome, halafu kama kuna cha kumjibu nifanye hivyo. Karibu ndani." Farida alimkaribisha sebuleni mgeni wake.

Hakutaka kuisoma pale mbele ya mgeni. Akaenda nayo chumbani. Akajifungia huku akitetemeka. Kwa sababu alijua lazima kuna jambo kubwa limeandikwa mle. Mtu ambaye umemtoroka wiki moja baada ya ndoa. Ambaye umemfedhehesha mbele za watu. Watu walioandaa sherehe, kucheza na kunywa, wote waje kujua kuwa bi harusi ametoroka. Si rahisi kuandika maneno rahisi.

Alianza kusoma. Baada ya dakika moja, machozi yalianza kumtoka. Kiliandikwa kila kitu. hakikuachwa kitu. Tangu walipoonana Kariakoo, kuoana, kutoroka, na cha zaidi, Tom aliandika sababu za Farida kuondoka. Kuna kipengele kimoja ambacho Farida alikiona ni muhimu na alikijutia.

"Kama ilikuwa ni hivyo ungeniambia kuwa una jamaa ambaye hataki kukuoa, halafu hataki kuona unaolewa. Ningejua cha kufanya. Kwangu lilikuwa ni tatizo dogo. Ambacho ningefanya ni kuruhusu kuondoka, lakini tungeweka mtego wa kumkatama kutokana na maneno yake na meseji za vitisho ambavyo alikuwa anakuandikia. Wala asingethubutu kuposti picha yoyote mbaya. Lakini uliogopa kuniambia, ukadhani sitokuelewa. Na ndiyo maana umesababisha yote haya."

Maneno hayo ni kama yalikuwa yamemfungua macho Farida. Alianza kujiona mjinga. Lakini akirudisha akili yake nyuma kwa wakati huo alidhani kuwa ni jambo ambalo lisingewezekana. Alidhani mumewe asingeweza kukubali. Kwanza angemuona kumbe ana mwanaume, kitu ambacho hakutaka kijulikane.

Aliangua kilio. Alikumbuka mengi. Cha zaidi kuwa siri yote ambayo alikuwa ameiweka mumewe asijue ilijulikana.

Alipomaliza kulia peke yake, alitoka sebuleni kwa mgeni wake.

"Nashukuru sana. Ila shoga yangu mimi sitoandika chochote. Nitakwambia tu nenda kwamwambie atafute mke mwingine aoe, mimi sikuwa chaguo sahihi kwake."

"Mhh, shoga kwa nini unasema hivyo jamani?"

"Kuna matatizo mengi kwenye ndoa yangu. Sijaitumikia chochote. Nilimtoroka wiki moja kabla baada ya ndoa. Na kisa ni kwamba kabla yake kulikuwa na mwanaume ambaye niliishi naye kama mpenzi wangu kwa mda mrefu. Hakuonioa. Iliniudhi, nikaamua kuondoka Morogoro kwenda Dar. Nikampata mtu. Mpenzi wangu wa Morogoro baada ya kujua, akaanza kunitisha kuwa anavijisha picha mbaya kwenye mitandao ya kijamii. Sikusikia. Nikaolewa, akanitisha tena, akaanza kunitumia mimi mwenyewe, nikaona zikifika kwenye mitandao nitakwisha, ndiyo nikamtoroka mume wangu." Alimhadithia Tedi kwa ufupi. Hakujua kama Tedi anafahamu kila kitu. Anamfahamu hadi Sam. Na si mgeni hapa Morogoro, ila ni mwenyeji ambaye alikuwa anafanya kazi ya uhudumu wa baa, ingawa kwa sasa Tom amemsimamisha na kumtawisha.

"Sasa shoga, kwani hilo ni kosa lako? Wanawake wakati mwingine tunakwenda kuolewa na wanaume wengine na kuwaacha wapenzi wetu wengine ambao tulikuwa nao kwa muda mrefu. Cha kufanya si umuombe mumeo msamaha?"

"Hapana. kwanza hata kama yeye atakubali, sidhani kama ndugu zake wanaweza kukubali. Pili Sam mwenyewe bado yupo, anaweza kufanya chochote kile."

Wakati wakiongea, Tedi alikuwa anawasiliana na Tom kwenye meseji. Ilikuwa ni saa 1:00 usiku. Mlango ukagongwa.

Ndugu mmoja wa Farida ndiye aliyekwenda kufungua. Wakati huo Farida na Tedi walikuwa wanaendelea kujadiliana.

Aliingia mgeni. Ni mgeni aliyesababisha kila mmoja ndani kushtuka, kasoro mmoja tu.

Alikuwa ni mwanaume mwenye umri wa miaka 40. Mweusi, mwenye nywele nyingi kichwani, mrefu mwembamba. Hakuwa mgeni sana kwenye nyumba hiyo. Si mwingine ni Tom.

Ulikuwa ni mwendelezo wa mpango mkakati kati yake ya Tedi. Kati ya wote, Farida ndiyo alikuwa kwenye mshtuko mkali zaidi. Hakuwahi kumuona mumewe tangu alipomtoroka Dar es Salaam, wiki moja baada ya ndoa.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KARATA NYINGINE MUHIMU KATIKA LIGI KUU BARA LEO

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya mapumziko ya wiki mbili kupisha kalenda ya kimataifa, kinyang'anyiro cha mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara kinarejea leo kwa Kagera Sugar kuwakaribisha Mbeya City kwenye Uwanja wa Kaitaba wakati Geita Gold itawavaa Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari ya Nyankumbu iliyoko mkoani Geita.

Zitakuwa ni mechi za raundi ya tatu za ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 na iliyoanza kuchezwa tangu Septemba 27, mwaka huu.

Geita Gold, baada ya kucheza mechi mbili ugenini, ikichapwa mabao 2-0 dhidi ya Namungo na bao 1-0 ilipokutana na Yanga, kwa mara ya kwanza baada ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara itacheza mechi nyumbani, jambo lililokuwa linasubiriwa mno na mashabiki na wapenzi wa mkoa huo wa Geita.

Timu zote mbili zinakutana zikiwa hazijaonja ladha yoyote ya ushindi kwenye ligi msimu huu, Geita Gold ikiwa haina pointi wala goli la kufunga, ikiburuza mkia, huku Mtibwa Sugar yenyewe ikiwa na pointi moja.

Hata hivyo, Mtibwa Sugar kama walivyo wenyeji wao, haijashinda mechi yoyote ya ligi, ikiwa imefungwa mechi moja dhidi ya Mbeya Kwanza bao 1-0 na mchezo wake wa pili ilitoka sare ya bila kufungana na Maafande wa Prisons, ikiwa ipo kwenye nafasi ya 12 ya msimamo.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, amekiri kuwa japo watakuwa nyumbani, lakini hawatakuwa kazi rahisi katika kusaka ushindi.

Baraza alisema kila timu imejipanga kusaka ushindi na wao kama wenyeji wamejiandaa kucheza kwa tahadhari na umakini ili wasipoteze mchezo huo.

Kocha huyo alisema kwake mechi zote ni muhimu na amewakumbusha wachezaji wake kucheza kwa nidhamu kwa sababu wapinzani wao wamejipanga kusaka ushindi pia.

"Tutajaribu kushinda, vijana wapo vizuri na wana ari ya kusaka matokeo mazuri, lakini tunakwenda kucheza na timu ambayo haijafanya vibaya kwenye mechi mbili za awali. Nawaomba tu mashabiki wa Kagera Sugar kujitokeza kuisapoti timu yao. Ligi imekuwa ngumu msimu huu kwa sababu timu zimepunguzwa, hivyo kila mechi ni fainali," alisema Baraza.

Kocha huyo aliongeza anahitaji kukusanya pointi nyingi kwenye mechi za mzunguko wa kwanza na hiyo itamsaidia kutokuwa na wasiwasi wa kushuka daraja watakapoingia kwenye hatua ya lala salama.

Kagera Sugar ina pointi moja kwenye nafasi ya 11, huku Mbeya City ikiwa kwenye nafasi ya nne kwa pointi nne.

Polisi Tanzania yenye makazi yake mkoani Kilimanjaro yenye pointi sita ndio inaongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo bingwa mtetezi wake ni Simba.




Ofisa Mtendaji wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Jacob Nduye, akimvisha medali mshindi wa kwanza wa mbio za Atlas Marathon, Augustino Sule, zilizofanyika katika viwanja vya Shule ya Atlas Madale, jijini Dar es Salaam juzi. Wa pili kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa shule hiyo, Sylivanus Rugambwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ufukweni Tanzania yaalikwa COSAFA

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Ufukweni inatarajia kushiriki mashindano ya kuwania ubingwa wa Kombe la COSAFA ambayo yamepangwa kufanyika kuanzia Novemba 8 hadi 15, mwaka huu nchini Afrika Kusini.

Tanzania inaenda kushiriki michuano hiyo kama timu mwalika baada ya kupanda katika viwango vya ubora duniani kutoka nafasi ya 72 hadi 42 na kwa ukanda wa Afrika ikipanda hadi nafasi ya saba baada kushiriki michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika huko Senegal. Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Pawasa, alisema kikosi chake kitaingia kambini keshokutwa Jumatatu na kambi yao itakuwa ya siku 15.

Pawasa alisema wakiwa katika mazoezi ya kujiandaa na mchezo huo, wanatarajia kucheza michezo mitatu ya kirafiki, miwili wakivaana na timu ya hapa nchini na mwingine mmoja utakuwa wa kimataifa na huenda ikawa ni Burundi.

Aliongeza mechi za Ligi ya Ufukweni inayoendelea imesaidia kuwapa nafasi ya wachezaji wake kujiimarisha na wengine kuonekana na kuita katika kikosi hicho.

Alitaja wachezaji watakaoingia kambini ni pamoja na makipa ni Adam Oseja, Andrew Ntala, Derick Charles na Hussein Mtagwa husu nafasi ya ulinzi ikiongozwa na Erick Manyama, Ismail Gambo, Ramadhan Said, Sadiq Salum na Nasoro Hussein.

Safu ya kiungo itaundwa na Jaruph Rajab, Mtoro Nasoro, Ally Kombo, Abdulkarim Kimombo, Salum Nyemba, Ibrahim Ibadi na Maulid Issah kwa washambuliaji ni Stephano Mapunda, Goodluck Aguero, Yahaya Tumbo na Hakhim Rajab.

## Bongozozo aanza majigambo ya tuzo

**Na Adam Fungamwango**

SHABIKI maarufu wa Timu za Taifa, Nickolaus Reynolds 'Bongozozo' ametamba atawashinda wapinzani wao, Haji Manara na Masau Bwire ambao wanawania Tuzo ya Mhamasishaji Bora inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imefahamika.

TFF inatarajia kutoa tuzo 56 kwa timu, klabu na viongozi waliofanya vyema kwa msimu wa 2019/20 katika sherehe maalum zitakazofanyika Oktoba 21, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mwalimu Nyerere jijini Dar es salaam.

Bongozozo amesema ingekuwa Tuzo hiyo ni kwa ajili ya Maofisa Habari angekuwa na wasiwasi, lakini kwa sababu imetajwa ni ya uhamasishaji, ana imani ataibuka mshindi kwa sababu hakuna yoyote kati ya wapinzani wake wawili anayempata kwa kuhamasisha, hasa kwenye timu ya Taifa, Taifa Stars.

"Kwanza kabisa ni heshima kubwa sana kwangu kuchaguliwa kuingia kwenye kuwania tuzo hiyo. Nilikuwa nina safari ya kwenda Oman," alisema Bongozozo.

Shabiki huyo amekiri Manara na Masau ni wazuri kwenye kuongea, lakini yeye ni mzuri kwenye kuhamasisha, kwani amekuwa akiifanya kazi hii kwa Taifa Stars akiwa ndani na nje ya nchi, huku akisafiri nayo nchi yoyote ile inapokwenda.

## Ihefu SC, African Lyon majaribuni

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupoteza michezo miwili ya Ligi ya Championship, Kocha Mkuu wa African Lyon, Khalid Adam amesema tayari ameshafanya marekebisho katika kikosi chake na anaamini wako tayari kupata matokeo mazuri katika mchezo wao unaofuata dhidi ya Ihefu SC.

African Lyon inatarajia kushuka ugenini leo kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali jijini Mbeya ili kuwakabili wenyeji Ihefu.

Akizungumza na gazeti hili, Adam alisema tayari amesahihisha makosa yaliyoonekana kwenye michezo miwili iliyopita na sasa kikosi chake kiko imara kuondoka na ushindi lakini wakiwaheshimu wapinzani wao.

Adam alisema mechi itakuwa na ushindani kwa sababu wamejipanga kwenda kutafuta matokeo chanya na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Tunaenda kupambana, nimeimarisha kikosi changu, ikiwamo safu ya ulinzi kuitaka iwe makini na mabeki wetu kuwa na utulivu katika kuwakaba washambuliaji wa wapinzani ili wasilete madhara ya kuwafunga," aliongeza kocha huyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LEWANDOWSKI ATAJWA

WAKALA wa Roberto Lewandowski, Pini, anaona Manchester City kama klabu ambayo mshambuliaji huyo wa Bayern na Poland mwenye umri wa miaka 33 anaweza kuhamia msimu ujao. **(Bild)**

### STERLING AGEUKA LULU

REAL Madrid, Newcastle United, Arsenal na Liverpool ni miongoni mwa klabu ambazo mshambuliaji wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 26, anaweza kujiunga nazo baada ya kutangaza kuwa yuko tayari kuondoka Manchester City. **(Express)**

### MAZRAOUI ANUKIA ARSENAL

LEEDS United inamfuatilia kwa karibu mlinzi wa Morocco na Ajax mwenye umri wa miaka 23, Noussair Mazraoui, ambaye pia amehusishwa na Arsenal na AS Roma. **(Football Insider)**

### SANCHES APATA BARAKA

RAIS wa Lille, Olivier Letang amefichua kuwa kiungo wa kati wa Ureno, Renato Sanches mwenye umri wa miaka 24, ataruhusiwa kuondoka klabu hapo ikiwa timu kubwa itawasilisha ofa ya kumnunua ifikapo Januari mwakani. **(Express)**

### GREEN ANUKIA SPURS

KLABU za West Ham na Tottenham Hotspur zimehusishwa na kipa wa Saint-Etienne, Etienne Green mwenye umri wa miaka 21, ambaye ni raia wa Ufaransa. **(TeamTalk)**

### FEKIR ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United wamewasiliana na wawakilishi wa kiungo wa kati wa Real Betis na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Nabil Fekir mwenye umri wa miaka 28. **(Footmercato)**

### NYOTA WA CHELSEA SOKONI

MLINZI wa Timu ya Taifa ya Hispania, Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 32 na mchezaji mwenzake wa Chelsea, Andreas Christensen (25), ni miongoni mwa wachezaji ambao wanawindwa na Barcelona kwa usajili msimu ujao. **(Fichajes)**

### LINGARD SAFARI IMEIVA

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Jesse Lingard (28), yuko tayari kuondoka klabuni hapo Januari ili kuimarisha nafasi yake ya kuteuliwa katika kikosi cha Timu ya Taifa ya England kitakachokwenda kwenye fainali za Kombe la Dunia mwakani. Barcelona na AC Milan wamehusishwa na uhamisho wa mchezaji huyo. **(Mirror)**

### LIVERPOOL YAMWANIA RAPHINHA

LIVERPOOL wameonyesha ishara ya kutaka kumsajili winga wa Leeds United na Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 24, wakati wa uhamisho wa msimu wa joto, wakala wa mchezaji huyo amedokeza. **(Globo Esporte)**

### ARTETA AMTAKA AARONS

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ana orodha ya wachezaji anaowahitaji ambayo inawajumuisha Tariq Lamptey mwenye umri wa miaka 21 kutoka Brighton, James Justin (Leicester City) na Max Aarons wa Norwich. **(Fichajes)**

### SESSEGNON HUYO UTURUKI

KLABU ya Fenerbahce inatafakari uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur na England, Ryan Sessegnon mwenye umri wa miaka 21, ifikapo Januari. **(Sun)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# STERLING ASEMA YUKO NJIA MOJA

**Nyota huyo ataja sababu kuu ni kuhitaji nafasi ya kucheza na kunusuru...**

**MANCHESTER, England**

RAHEEM Sterling amewekwa "wazi" uamuzi wa kutaka kuondoka kutoka Manchester City ili apate sehemu ya kucheza mara kwa mara.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 aling'ara katika kikosi cha Timu ya Taifa ya England kilichoshiriki ya Euro 2020, akifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho 10 kuelekea katika hatua ya fainali, ambapo walifungwa na Italia.

Licha ya Sterling kuonyesha kiwango cha kuvutia kwa nchi yake, kwenye ngazi ya klabu, kocha wake, Pep Guardiola amekuwa hamtumii mara kwa mara msimu huu, akimpa winga huyo dakika 274 katika mechi za Ligi Kuu England hadi sasa.

Katika dakika hizo, ameanza kwenye mechi mbili tu kati ya saba za Ligi Kuu England msimu huu.

Sterling sasa ameonyesha ishara ya utayari wa kuondoka, huku mkataba wake ukiwa unamalizika msimu ujao.

"Kama kutakuwa na ulazima wa mimi kuondoka na kwenda sehemu nyingine ambako nitapata nafasi ya kucheza mara kwa mara, nitakuwa tayari," alisema Sterling akiliambia gazeti la Financial Times. "Kama nilivyosema, soka ni kitu muhimu zaidi kwenye maisha yangu, kwani haya ndio maisha yenyewe kwangu mimi."

MECHI KALI
HOME
AWAY
LEICESTER
3.32 | 3.47 | 2.15
MANCHESTER UTD
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 576
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MESSI AMJIA JUU MWAMUZI

**BUENOS AIRES, Argentina**

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, alimbwatukia mwamuzi, licha ya mabingwa hao wa Copa America kuibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Peru kwenye michuano ya kufuzu Kombe la Dunia.

Bao la kichwa la Lautaro Martinez zikiwa zimesalia dakika mbili kabla ya mapumziko katika mchezo huo uliopigwa jijini Buenos Aires juzi, liliwapa ushindi La Albiceleste hao na sasa wamefikisha mechi 25 bila kupoteza kwenye mashindano yote.

Peru walikosa nafasi ya kupata pointi moja baada ya Yoshimar Yotun kupaisha penati yake zikiwa zimesalia dakika 25 mchezo kumalizika.

Messi alionekana kumbwatukia mwamuzi licha ya kutosikika alichokuwa akizungumza wakati Martinez alipokuwa ameanguka eneo la hatari kipindi cha kwanza.

"Mechi ngumu, ngumu kucheza. Upepo mwingi, walikuwa wanacheza kwa kutukamia sana na tulipata nafasi chache," aliandika Messi kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Mwamuzi mara zote alikuwa haangalii makosa ya wapinzani wetu, alionekana kama alikuwa akifanya makusudi tu.

"Lakini jambo la msingi ni kwamba tumepata pointi tatu na tunakaribia kufikia malengo yetu."

Martinez hilo lilikuwa bao lake la 17 kwenye timu ya taifa na fowadi huyo wa Inter Milan ndio mfungaji bora wa kikosi cha Argentina chini ya kocha wa sasa, Lionel Scaloni, ukiacha Messi ambaye ni mfungaji wa wakati wote wa kikosi hicho.

Scaloni sasa amekuwa kocha wa pili wa Argentina katika historia ya timu ya taifa kuiongoza timu hiyo kushinda mechi 25 mfululizo kwenye mashindano yote baada ya Alfio Basile.

# Fabinho alitarajia Raphinha kutua Liverpool



**SAO PAULO, Brazil**

FABINHO amesifia kiwango cha Raphinha tangu awasili kwenye Ligi Kuu England na kusema alitarajia winga huyo wa Leeds United kujiunga na Liverpool mapema mwaka huu.

Raphinha mwenye umri wa miaka 24 ameng'ara Leeds tangu alipotua hapo akitokea Rennes kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 17 hapo Oktoba, mwaka jana na aliichezea mechi yake ya kwanza Brazil wiki iliyopita.

"Tangu alipowasili kwenye Ligi Kuu England, amekuwa kwenye kiwango bora pale Leeds," alisema Fabinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Hata wakati wa soko la uhamisho wa majira ya joto, kulikuwa na mazungumzo kwamba anaweza kwenda Liverpool.

"Nilitarajia hilo lingetokea, lakini alibakia Leeds."

Wakala wa Raphinha, Deco amethibitsha kwamba, Liverpool walionyesha nia ya kutaka kumsajili winga huyo wakati wa madirisha la uhamisho wa hivi karibuni.

"Ni mchezaji muhimu," alisema Deco akiliambia gazeti la Brazil la O Globo. "Kulikuwa na klabu kadhaa zilioonyesha nia ya kumtaka yeye na Liverpool inamtaka."

6,086,780

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 16/10/21 | 17:00 | Southampton vs Leeds | 2.40 | 3.52 | 2.82 |
| 02. 16/10/21 | 17:00 | Blackburn vs Coventry | 2.81 | 3.11 | 2.52 |
| 03. 16/10/21 | 17:00 | Millwall vs Luton Town | 2.30 | 3.20 | 3.06 |
| 04. 16/10/21 | 17:00 | Girona vs Huesca | 2.44 | 2.87 | 3.16 |
| 05. 16/10/21 | 19:15 | Las Palmas UD vs Tenerife | 2.51 | 2.95 | 2.95 |
| 06. 16/10/21 | 19:30 | Levante vs Getafe | 2.56 | 2.91 | 3.11 |
| 07. 16/10/21 | 21:30 | Malaga vs Zaragoza | 2.53 | 2.97 | 2.92 |
| 08. 17/10/21 | 13:30 | Cagliari vs Sampdoria | 2.72 | 3.37 | 2.56 |
| 09. 17/10/21 | 14:00 | Swansea vs Cardiff | 2.44 | 3.06 | 2.96 |
| 10. 17/10/21 | 16:00 | Everton vs West Ham | 2.38 | 3.42 | 2.92 |
| 11. 17/10/21 | 16:00 | Bordeaux vs Nantes | 2.78 | 3.13 | 2.59 |
| 12. 17/10/21 | 16:00 | Udinese vs Bologna | 2.36 | 3.35 | 3.00 |
| 13. 17/10/21 | 17:00 | Leganes vs Valladolid | 2.46 | 2.97 | 3.02 |

MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 16 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4591 | Watford vs Liverpool | 7.59 | 5.19 | 1.37 |
| 14:30 | 4685 | Fulham vs QPR | 1.60 | 4.06 | 4.95 |
| 16:00 | 1869 | Spezia vs Salernitana | 2.16 | 3.36 | 3.41 |
| 16:30 | 2160 | Greuther Furth vs VfL Bochum | 2.38 | 3.40 | 2.85 |
| 16:30 | 2345 | Union Berlin vs VfL Wolfsburg | 2.68 | 3.13 | 2.68 |
| 16:30 | 5266 | Eintracht Frankfurt vs Hertha BSC | 1.71 | 3.83 | 4.57 |
| 16:30 | 5882 | Borussia Dortmund vs Mainz | 1.41 | 5.00 | 6.40 |
| 16:55 | 5031 | Kolubara vs Red Star Belgrade | 13.57 | 6.79 | 1.14 |
| 17:00 | 1213 | Leicester vs Manchester Utd | 3.32 | 3.47 | 2.15 |
| 17:00 | 1822 | Motherwell vs Celtic | 6.11 | 4.34 | 1.47 |
| 17:00 | 2115 | Blackburn vs Coventry | 2.71 | 3.16 | 2.57 |
| 17:00 | 2542 | Huddersfield vs Hull City | 1.98 | 3.31 | 3.75 |
| 17:00 | 2735 | Aston Villa vs Wolverhampton | 2.25 | 3.22 | 3.32 |
| 17:00 | 3078 | Nottingham vs Blackpool | 2.00 | 3.25 | 3.74 |
| 17:00 | 3086 | Sheffield Utd vs Stoke City | 2.18 | 3.20 | 3.30 |
| 17:00 | 3094 | Bristol City vs Bournemouth | 4.14 | 3.45 | 1.84 |
| 17:00 | 3910 | St Johnstone vs Livingston | 1.85 | 3.25 | 4.43 |
| 17:00 | 3924 | Rangers vs Hearts | 1.56 | 4.07 | 5.35 |
| 17:00 | 4425 | Norwich City vs Brighton | 3.61 | 3.31 | 2.10 |
| 17:00 | 4778 | FK Lviv vs Dynamo Kiev | 10.62 | 5.60 | 1.22 |
| 17:00 | 5372 | Preston vs Derby | 2.02 | 3.06 | 3.95 |
| 17:00 | 5664 | Ross County vs St Mirren | 3.06 | 3.31 | 2.24 |
| 17:30 | 3123 | Ludogorets Razgrad vs Tsarsko Selo | 1.13 | 6.78 | 15.49 |
| 18:00 | 4095 | Clermont Foot vs Lille | 3.08 | 3.33 | 2.27 |
| 18:00 | 4601 | SCR Altach vs RB Salzburg | 12.50 | 6.73 | 1.15 |
| 18:15 | 3729 | Apollon Smyrnis vs Asteras Tripolis | 2.86 | 3.06 | 2.51 |
| 18:30 | 2972 | Kaizer Chiefs vs Chippa Utd | 2.20 | 2.95 | 3.70 |
| 19:00 | 3610 | BSC Young Boys vs FC Luzern | 1.24 | 6.33 | 9.29 |
| 19:00 | 3728 | Sochi vs Rostov | 1.73 | 3.55 | 4.63 |
| 19:00 | 3904 | Lillestrom vs Kristiansund | 1.90 | 3.59 | 3.69 |
| 19:00 | 4504 | Spartak Moscow vs Dinamo Moscow | 2.46 | 3.20 | 2.81 |
| 19:00 | 4970 | Yverdon-Sport FC vs FC Wil | 1.97 | 3.78 | 3.10 |
| 19:00 | 5223 | Adana Demirspor vs Yeni Malatyaspor | 1.72 | 3.80 | 4.35 |
| 19:00 | 5782 | Lazio vs Inter | 3.27 | 3.47 | 2.17 |
| 19:30 | 1278 | Levante vs Getafe | 2.51 | 2.91 | 3.21 |
| 19:30 | 1387 | Monchengladbach vs Stuttgart | 1.51 | 4.58 | 5.38 |
| 19:30 | 1769 | Glentoran Belfast vs Coleraine FC | 2.01 | 3.58 | 3.14 |
| 19:30 | 2556 | Brentford vs Chelsea | 5.83 | 3.87 | 1.60 |
| 19:30 | 2791 | Zulte Waregem vs Royal Antwerp | 4.16 | 4.16 | 1.68 |
| 19:30 | 3544 | Oostende vs Cercle Brugge | 2.11 | 3.65 | 3.06 |
| 19:30 | 5378 | SC Dnipro 1 vs Kolos Kovalivka | 1.60 | 3.78 | 4.85 |
| 19:45 | 4272 | GO Ahead Eagles vs Heracles Almelo | 2.96 | 3.40 | 2.26 |
| 19:45 | 5097 | Heerenveen vs Ajax | 9.84 | 6.50 | 1.22 |
| 20:00 | 5745 | Dundee FC vs Aberdeen | 2.82 | 3.21 | 2.45 |
| 20:30 | 2887 | Panathinaikos vs Ionikos Nikea FC | 1.47 | 4.14 | 6.51 |
| 21:30 | 5245 | FC Zurich vs FC Lugano | 2.02 | 3.55 | 3.35 |
| 21:45 | 3273 | AC Milan vs Verona | 1.58 | 4.33 | 5.23 |
| 22:00 | 1382 | Real Sociedad vs Mallorca | 1.44 | 4.44 | 7.27 |
| 22:00 | 3151 | PSV Eindhoven vs PEC Zwolle | 1.14 | 7.50 | 14.79 |
| 22:00 | 3755 | Fortuna Sittard vs Cambuur | 2.51 | 3.50 | 2.56 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# PEDRI AJIFUNGA BARCA HADI 2026




**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa Hispania, Pedri amesaini mkataba mpya wa muda mrefu na klabu yake ya Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 alikuwa amebakiwa na chini ya miezi 12 kwenye mkataba wake wa sasa ingawa klabu hiyo ilikuwa na kipengele cha kumwongezea kwa misimu mingine miwili.

Na badala yake wameamua kumpa mkataba wa muda mrefu, ambapo kiungo huyo atabakia kwa miamba hao wa Katalunya hadi mwaka 2026.

Taarifa ya Barca ilisomeka: "FC Barcelona na mchezaji Pedro 'Pedri' Gonzalez imefikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya ambao utamalizika Juni 30, mwaka 2026.

"Kipengele cha kukatisha mkataba huo kina thamani ya euro bilioni moja."

Pedri amepata uzoefu haraka tangu alipojiunga na Barca akitokea Las Palmas mwaka jana, na kujiimarisha yeye mwenyewe kama mchezaji muhimu akitokea kwenye timu B ya Blaugrana hao.

Alikuwa kivutio kikubwa kwa kocha wake, Ronald Koeman kwenye msimu mpya wa maandalizi.

Koeman alimtumia Pedri katika mechi 37 msimu uliopita, akilingana na Frenkie de Jong (pia mechi 37) ambao ni wachezaji waliocheza mechi nyingi zaidi kwa klabu hiyo.

# Lingard bado kuamua hatima yake



**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard bado anasoma 'upepo' kabla ya kuamua hatima yake ndani ya kikosi hicho, kwa mujibu wa Daily Mail.

Ripoti hiyo imedai Lingard amegoma kusaini mkataba mpya wa kuendelea kubaki United licha ya uongozi wa klabu hiyo kumtaka mchezaji huyo kusalia kikosini hapo.

Inasemekana suala linalomvuta nyuma Jesse, ni uwepo wa wachezaji wawili - Jadon Sancho na Cristiano Ronaldo.

Usajili wa wachezaji hawa, ni dhahiri umeongeza ushindani wa namba kwenye kikosi cha Solsksjaer na hivyo ni sahihi kwa Lingard kuangalia nafasi yake ya muda mrefu kwenye kikosi hicho cha Mashetani Wekundu.

Mkataba wa Lingard na Manchester United unamalizika mwishoni mwa msimu huu na kumekuwa na uhusishwaji wa baadhi ya klabu kuwania saini ya mchezaji huyo.

Klabu za Barcelona na AC Milan ni miongoni mwa timu zinazohusishwa na saini ya Lingard.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 16, 2021
Nipashe



Sterling asema yuko njia moja

UKURASA 21

# GOMES AFUNGUKA USHINDI NI LAZIMA

**Huku Biashara United ikiwaduwaza Al Ahly Tripol na kujiweka katika...**

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

SAFARI imeanza, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes ambaye jana jioni aliongoza kikosi cha timu hiyo kuelekea Botswana kwa ajili ya mechi ya raundi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy itakayochezwa kesho nchini humo.

Gomes aliliambia gazeti hili wanakwenda Botswana kusaka ushindi na malengo yao ni kupata matokeo mazuri na hatimaye kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Kocha huyo alisema anatarajia kukutana na ushindani katika mechi hiyo na amewaona wachezaji wa Jwaneng Galaxy wana uwezo wa kushambulia na baadaye kurejea haraka kuimarisha safu ya ulinzi.

Alisema wanafahamu mechi hiyo haitakuwa nyepesi kwa kila upande kwa sababu kila timu inahitaji kushinda na kujiweka kwenye mazingira mazuri kuelekea mchezo wa marudiano ambayo utachezwa Oktoba 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

"Tunakwenda kupambana kusaka matokeo mazuri, si mchezo mwepesi kwa Simba au kwa wapinzani wetu, kwa sasa tunahitaji kupata matokeo mazuri na kutinga hatua ya makundi, naamini tutafanya vizuri," alisema kocha huyo.

Naye nahodha wa Simba, John Bocco, alisema wanakwenda Botswana kwa kazi moja ya kupambana kwa ajili ya timu yao na vile vile kupeperusha vyema bendera ya Tanzania.

"Tunahitaji kupata ushindi, tunajua hakuna timu ndogo, kila upande umejiandaa kwa ajili ya kusaka ushindi, hatutabweteka," Bocco alisema.

Naye Mratibu wa Simba, Abbas Ally ambaye alitangulia Botswana alisema mapokezi kwa ajili ya kikosi hicho yamekamilika na wamejipanga kukabiliana na hali ya hewa ya joto iliyoko nchini humo.

Wachezaji wa Simba walioondoka nchini jana kuelekea Botswana ni pamoja na Aishi Manula, Beno Kakolanya, Ally Salum, Shomary Kapombe, Israel Mwenda, Mohamed Hussein, Gadiel Maichael, Erasto Nyoni, Pascal Wawa, Kennedy Juma, Inonga Varane, Joash Onyango, Thadeo Lwanga, Jonas Mkude, Sadio Kanoute, Rally Bwalya, Mzamiru Yassin, Ibrahim Ajibu, Hassan Dilunga, Bernard Morrison, Peter Banda, Duncan Nyoni, Meddie Kagere na Bocco.

Wakati huo huo Biashara United imejiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kuifunga Al Ahly Tripoli mabao 2-0 katika mchezo wa michuano hiyo uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. Biashara United ilikwenda mapumziko ikiwa mbele kwa bao 1-0, shukrani kwa Judica Mafie aliyeingia dakika ya 39 na Atupele Green ambaye alitikisa nyavu za Waarabu hao wa Libya.

Dakika 20 za mwisho za mchezo huo zilikuwa ngumu kwa wenyeji kutokana na Al Ahly kufanya mashambulizi ya mara kwa mara, lakini hayakuzaa matunda.

Timu hizo zitarudiana Oktoba 24, mwaka huu nchini Misri na hiyo inatokana na Libya kutokuwa salama.



Mshambuliaji wa Biashara United, Atupele Green (aliye juu), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Al Ahly Tripoli katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. Biashara United ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga yapeleka shangwe Songea

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikitarajiwa kuondoka jijini Dar es Salaam kesho ili kuelekea Songea, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nesreddine Nabi amesema anatengeneza kikosi imara kitakachowapa raha mashabiki na wanachama wa timu hiyo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC itakayochezwa Jumanne.

Nabi aliliambia gazeti hili amefurahishwa na kurejea kwa nyota wake wawili, David Bryson na Yassin Mustafa ambao walikuwa majeruhi na sasa wameongeza nguvu katika safu yake ya ulinzi.

Alisema wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na hana presha yoyote katika safu ya ulinzi kwa sababu kurejea kwa nyota hao kumeimarisha timu hiyo na kuwa mkali kwa washambuliaji wake kucheza kwa ushirikiano wenyewe kwa wenyewe.

"Sina presha kwenye safu yangu ya ulinzi tumeimarika vizuri, nimekuwa mkali kwa washambuliaji na kuwataka kufanya kazi kwa ushirikiano bila kuangalia mafanikio ya mtu binafsi katika kutengeneza nafasi na kufunga,".

"Nimeona katika michezo yote tuliyocheza, washambuliaji walikuwa kila mmoja akitaka kufunga, nimekuwa mkali siku zote inashinda timu anafunga au anatengeneza nafasi mchezaji," alisema Nabi.

Aliongeza wanahitaji kuendeleza kasi ya ushindi ili kujiweka kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo unaoongozwa na Polisi Tanzania.

"Tumejipanga vizuri na kikosi kipo tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri katika mchezo wetu huo, KMC FC sio timu mbaya, wamejipanga vizuri na nina imani utakuwa mchezo wenye ushindani mkubwa kwa pande zote mbili," alisema Kocha huyo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga iko katika nafasi ya pili ikiwa na pointi sita sawa na vinara wakati mabingwa watetezi Simba yenye pointi nne wako katika nafasi ya nne.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002